Yawaletea

NENO NA ROHO

Huduma katika Nguvu za Roho Mtakatifu

Kusanyiko la mafundisho

Yaliyoandaliwa na

MTUME PAUL GALLIGAN

YALIYOMO

Sura ya Kwanza **Wokovu**
Utajuaje umeokoka
Wokovu
Tumeokolewa kwa imani
Tumeokolewa kwa damu
Tumeokolewa katika Roho

Sura ya Pili **Neno la Mungu**
Neno la Mungu katika Mwanzo
Yesu ni Neno
Mbegu ya Neno
Maziwa ya Neno
Nyama ya Neno
Kila Andiko lina Pumzi ya Mungu
Kufundishwa katika Neno

Sura ya Tatu **Roho Mtakatifu ni Nani?**
Ahadi ya Baba
Roho Mtakatifu katika ulimwengu
Yesu na Roho Mtakatifu
Yesu alinena kuhusu kuja Kwa Roho Mtakatifu
Agano Jipya katika Roho
Roho Mtakatifu ni Mtu

Sura ya Nne **Roho Mtakatifu Anakuja: Jinsi ya kujazwa**
Roho Mtakatifu alikuja vipi?
Ni lini wanafunzi walizaliwa mara ya Pili?
Ninampokeaje Roho Mtakatifu?
Roho Mtakatifu anafananaje?
Yesu anayebatiza kwa Roho Mtakatifu
Kunena kwa Lugha Mpya

Sura ya Tano **Karama za Roho Mtakatifu**
Karama tisa za **1 Kor.12:8-10**
Kuhudumu katika karama

Sura ya Sita **Kuendelea hadi tuufikilie utimilifu**
Kanisa linafikiaje utimilifu
Vipawa vya huduma tano
Huduma za kila sehemu

Sura ya Saba **Karama saba za Baba katika Rum. 12**
Unabii, Huduma, Kufundisha, Kuonya, Kutoa, Uongozi, Kurehemu.

SURA YA KWANZA
WOKOVU

Luka 19:1-10 inanakili hadithi ya Zakayo alivyompokea Yesu katika nyumba yake kama mgeni, akimtambua kama Bwana, na kujitolea kufanya marekebisho katika makosa yake kama mtosa ushuru. Yesu akamwambia, "***leo wokovu umefika nyumbani humu.”*** Ni hadithi ya toba na imani iletayo wokovu. Zakayo alikuwa amesikia habari kuhusu Yesu. **Rum 10:17** inatwambia kwamba imani huja kwa kusikia.

Zakayo aliwezaje kuokoka?:

1. Baada ya kusikia habari kuhusu Yesu, alitamani kumuona;
2. Yesu alikutana na Zakayo, akiitikia imani iliyokuwa ndani ya moyo wa Zakayo;
3. Yesu aliingia nyumbani mwake;
4. Zakayo alimpokea Yesu; alikuwa na kubadili nia, na akaitikia Neno la Yesu.
5. Yesu alitangaza wokovu kwa sababu aliona imani katika moyo wa Zakayo, na akamsikia Zakayo akikiri kwamba atarejesha kile alichokuwa ameiba.

Yohana 1:12 Inatwambia kwamba tunazaliwa mara ya pili wakati tunapompokea Yesu baada ya kuliamini Jina Lake.
Rum.10:9-19 inatwambia kwamba imetupasa kuamini mioyoni mwetu kwamba Mungu alimfufua Yesu kutoka katika wafu, na kukiri kwa vinywa vyetu kwamba Yes uni Bwana. Hapo ndipo tutaokoka.

> **Wokovu: neno linalomaanisha**
> **Tafsiri ya Maneno ya Biblia #4991 Gr, *Soteria,* kumaanisha kuokoa ama usalama;**
> **Limetafsiriwa: komboa, afya, wokovu, okoa, kuokoa**
> **Linatokana na neno *Soter,* mkombozi, na neno *Sozo,* kuokoa, kulinda, kukomboa**
> **Linganisha na SC #3444 Heb, *yeshooaw,* kitu kilichookolewa, ukombozi, msaada,ushindi, ufanisi. Vipengee vyote vya hili neno ni sehemu ya wokovu wetu. Yesu analeta wokovu kwa mtu kwa jumla.**

UTAJUAJE UMEOKOKA?
Kumbuka ulipookoka!
Ni nini kilichotendeka ndipo ujue umeokoka?
Ili tendekaje?
Unafanya nini wakati mashaka yanapokujia wokovu wako?

Biblia inasema nini? Ni kuamini tu na kukiri.
Rum.10:8 ***“Neno li karibu nawe, kinywani mwako na katika moyo wako [yaani neno la imani tulihubirilo]”***
a.9 ***Kiri*** kwa kinywa chako kile ambacho unaamini kwa moyo wako.
a.10 ***Amini*** kwa moyo wako katika haki na ukiri wokovu wako.
a.11 tunapomtumainia Bwana, Anatuondoa aibu.
a.12 Bwana ni mwingi wa utajiri kwa wale wamwitao.
a.13 ***Ye yote*** atakaye liitia Jina la Bwana ataokoka.

Kushinda mashaka kwa njia ya imani
Tunatambua kwamba mashaka huja katika nia zetu, lakini imani hutoka moyoni. **Efe.6:16** inatwambia kuvaa nago ya imani [kile ambacho tunaamini na kukiri] na tukabiliane na mashaka.
Kum.30:14 ***“Lakini Neno li karibu nawe, katika kinywa chako na moyo wako, upate kulifanya.”***

Tunaamini nini?

1. Tunamwamini Yesu. **Yoh.14:1** Aminini Yesu; **Yoh.6:29** Amini Yule ambaye Mungu ametuma.
2. Amini kutiwa nguvu na Roho Mtakatifu. **Lu.24:49** Yesu aliahidi Roho Mtakatifu; **Matendo 1:8** you will receive power.

WOKOVU

Tufanye nini ili tupate kuokoka

Mk.1:15 Yesu alisema ***"Tubuni na Mwamini katika Injili."***
Acts 3:19 Petro alisema ***"Tubuni basi, na mrejee, ili dhambi zenu zifutwe."***
Acts 20:21 Paulo alisema ***"Wamtubie Mungu na kumwamini Bwana wetu Yesu Kristo."***
Mk.16:16 Yesu alisema ***"Aaminiye na kubatizwa ataokoka."***
Ili tupate kuokoka itatubidi kutubu dhambi zetu na tuamini Injili.
Lazima tumgeukie Mungu na kuamini katika Kristo
Lazima tugeuke kutoka kwa kazi zisizo na uhai za dini;
Yatupasa kuamini na kubatizwa!

Tunaokoka jinsi gani?

A) **Tunaokolewa kwa imani**, ni kipawa cha Mungu **Efe.2:8**.
B) **Tunaokolewa kwa damu**, sadaka ya upatanisho **Efe.2:13, Ebr.9:12**.
C) **Tunaokolewa kwa Roho mmoja, Efe.2:18, Yoh.3:5-6**

A) TUNAOKOLEWA KWA IMANI

Imani huja vipi?

1. *Kwa kusikia neno linalonenwa* [rhema] Neno la Mungu. **Rum.10:17** Watu wengi ambao wamekuja kwa imani, wamemsikia mtu akiongea kuhusu Yesu Kristo. Hili ndilo neno linenwalo *'rhema'*, amblo ndilo Neno la Mungu lililowekwa tayari kwa ajili yetu. Mara tu tunaposikia, tunaamini; kisha 'tunakiri' kwa vinywa vyetu.(**Rum.10:9-10**)

Kusikia → Kuamini → Kukiri

2. *Kwa kuamini Neno la Mungu lililoandikwa* [logos]. **Yoh.20:31** Injili ya Yohana na waraka wa kwanza wa Yohana, hunena zaidi juu ya kuamini katika Mwana wa Mungu. Kwa njia ya kuamini utapata uzima, utaujua ukweli na kumjua Mungu Baba kupitia kwa Yesu Kristo.

3. *Ufahamu wa imani kutoka Mwanzo* [Mwanzo ni kitabu cha mbegu ya Biblia].

Mbegu ya ahadi

Mungu aliponena na Adamu na Hawa baada ya wao kula tunda walilokatazwa, Hawa alimlaumu nyoka kwa kumdanganya (**Mwa.3:13**). Katika **Mwa.3:15** Mungu anaahdi kwamba **Mbegu** ya mwanamke itaponda kichwa cha shetani. Huu ndio mwanzo wa kuhubiri Injili, kutabiri juu ya kuja kwake Masihi, na kuongea kuhusu vita kati ya Yesu na shetani Yesu akiwa Mshindi.

Mwa.3:20 Adamu alikwa na imani, aliamini kile Mungu alisema na katika imani akamwita mkewe Hawa, *'mama wa wote walio hai'.*

Mwa.3:21 Damu ya kwanza ilimwagwa na Mungu kufunika dhambi ya Adamu na Hawa na akwatengenezea mavazi kutoka kwa ngozi ya mnyama. Aliufunika **"uchi"** wao.

Mbegu ya Mwanamke ambayo Mungu alinena juu yaka ni Yesu Kristo. Kristo [Masihi] alizaliwa na mwanamke (**Gal.4:4**).

Ibrahimu

Ibrahimu alipewa ahadi kuhusu Yule atakayetoka katika mwili wake [**mbegu**] ambaye atakuwa Baraka kwa mataifa yote. **Mwa.12:3** ***"na katika wewe jamaa wote wa duniani watabarikiwa."***
Mwa.15:2-6 Ibrahimu alikuwa hana mwana hata japo Mungu alikuwa amemwahidi mrithi.

Mungu alisema ***"Yule atakayetoka katika mwili wako ndiye atakayekuwa mrithi wako".*** Ibrahimu aliaminim Mungu na BWANA akamhesabia hilo kuwa haki (**a.6**). Ibrahimu alikuwa mtu wa imani. **Mbegu** aliyoahidiwa Hawa na **mbegu** aliyoahidiwa Ibrahim uni moja ambayo ni kuja kwake Yesu Kristo (**Gal.3:16**). Na kupitia kwa Yesu Kristo ahadi ya Mungu inatolewa kwa wote waliondani ya Kristo ***"na ikiwa ninyi ni waKristo, basi ninyi ni uzao wa Ibrahimu, na warithi kulingana na ahadi"*** **Gal.3:29**. Ibrahimu aliamini ***"katika tumaini pasipo tumaini"*** **Rum.4:18**.

WOKOVU = UZIMA WA MILELE
Yoh.3:16-17 Inaahidi nini? Tunapokea uzima wa milele kwa kuamini ushuhuda wa Neno la Mungu kuhusu Yesu Kristo. Mara tunapomwamini Yesu Kristo tunawezeshwa kumpokea na ***"Mungu anatupatia uwezo wa kufanyika watoto Wake"*** **Yoh. 1:12**.

YESU KRISTO NDIYE FUNZO na MSINGI WA IMANI YETU.
Yoh.14:6 Tunakuja kwa Baba kupitia kwa Yesu.
Yoh.14:9 Tunamwona Baba katika Yesu.
Fil.3:3 Tunafurahi katika Kristo.
Fil.3:8-11 Hakuna kinachojalisha ila tu ***"kupatikana ndani Yake"*** na ***"kuufikia ufufuo wa wafu."***
Fil.3:14 Mungu ametuita ***"kuelekea juu"*** katika Kristo Yesu.
Fil.3:20 Wenyeji wetu wa mbinguni uko juu ya Yesu Kristo.
Efe.1:15-18 Ufahamu wetu wa tumaini ambalo tumeitiwa liko juu ya ***"imani yetu ndani ya Bwana Yesu"***.

Tumeokolewa kwa neema
Mwa.6:8 Nuhu ni mfano wa Yule aliamini Mungu katikati ya watu wasioamini. Alipata ***"neema machoni pa Mungu"***, maana Mungu alimshauri amjengee safina ya wokovu.
a.14 Nuhu alitii – imani yake ilimwongoza kwa matendo. ***Kusikia na kutenda ni Imani***.

LOGOS na RHEMA
Katika Agano Jipya, maneno mawili ya Kiyunani yanajitokeza ambayo hutafsiriwa kwa neno noja '***Neno'.*** Maneno hayo ya Kiyunani ni ***logos*** na ***rhema***.
Yoh.1:1 ***"Hapo mwanzo kulikuweko Neno [Logos]"***. Hapa **Logos** ni Yesu, Yeye ni Neno. Katika aya nyingine nyingi *logos* linatafsiriwa ***neno*** [karibu mara 200]. ***Logos*** linaashiria Biblia kuwa Neno la Mungu. ***Logos*** ni Neno la Mungu lililoandikwa, ambalo limenakiliwa kwa ajili yetu.
Matt.4:4 ***"Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu". Rhema*** ni neno lililohuishwa, neno la sasa, linalotoka katika kinywa cha Mungu. Ni neno la ***rhema*** ndilo huweka uhai imani ndani yetu **Rum.10:17**; ni Neno la ***rhema*** ndilo lililomo katika vinywa vyetu na mioyoni mwetu **Rum.10:8**; Ni Neno la ***rhema*** ndilo upanga wa Roho **Efe.6:17**.

B) TUNAOKOLEWA KWA DAMU

Mungu alipokuwa karibu kuwakomboa Waisraeli kutoka utumwani Misri, aliwaahidi kwamba **damu** katika nyumba zao ni ***"alama"*** (**Kut.12:13**). Aliahidi ***"kupita juu"*** ya hizo nyumba bila kuziharibu. **Damu** ilikuwa njia ya ukombozi kwa mtu binafsi, jamii na taifa.
Agano la Kale lililofanywa katika Mlima Sinai (**Kut.24:1-3**) linatiwa chapa na damu iliyoko kwenye madhabahu (**a.6**), halafu damu juu ya watu (**a.8**). Mungu aliahidi kukutana na wana wa Israeli kwenye Kiti cha Rehema (**Kut.25:22**) kwa sababu **damu** iliwekwa kwenye kiti cha rehema. Linganisha na **Ebr. 9:11-14.** Yesu, Kuhani wetu Mkuu alipeleka damu yake mwenyewe katika Patakatifu pa Mungu, na kuweka juu ya kiti cha Rehema mbinguni juu. Damu yake unafanya upatanisho wetu. Chini ya sheria ya Musa tunahatia na tunastahili

hukumu ya kifo lakini Yesu alikufa kwa ajili yetu na kupeleka damu Yake aliyomwaga sio hema ya Mungu iliyofanywa bila mikono ya mwanadamu.

Ebr.9:22 ***"Pasipo umwagikaji wa damu, hakuna ondoleo la dhambi."*** Damu ya Yesu iliyomwagika inatupatanisha na Mungu. Tunapoamini hilo ndipotunapokea uzima na kushinda dhambi. **Rum.5:9** ***"Basi zaidi sana, tukisha hesabiwa haki katika damu Yake, tutaokolewa na ghadhabu kwa Yeye."*** Tumekombolewa ***"kwa damu ya dhamani ya Yesu"*** **1Pet.1:19**.

Agano Jipya
Kwenye Chakula cha Bwana pamoja na wanafunzi wake, Yesu aliidhinisha Agano Jipya (**Matt.26:26-29**).
a.28 ***"Kwa maana hii ndiyo damu yangu ya Agano Jipya, ambayo imemwagika kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi."*** **Ebr.8:8-12** inaashiria agano hilo, na **Ebr.10:16-18** inazungumzia juu ya kudumu kwa dhabihu hiyo ya Yesu. **Yesu alikufa mara moja, kwa ajili ya wote.** Hakuna dhabihu nyingine inayohitajika.

C) TUMEOKOLEWA KWA ROHO MMOJA.

Ahadi ya kuja kwa Roho, kunaanza kutimia na kuzaliwa upya: ***"mtu asipozaliwa mara ya pilihawezi kuuona ufalme wa Mungu."*** **Yoh.3:3**. ***"Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuingia katika ufalme wa Mungu."*** **Yoh.3:5**. Tunapozaliwa kwa Roho wa Mungu ndipo tunaokolewa. Tunaamini katika mioyo yetu kwamba Yesu ametupatanisha na Mungu na ***"kwa yeye sisi sote tumepata njia ya kumkaribia Baba katika Roho Mmoja"*** **Efe.2:18**. Tunakiri kwa vinywa vyetu kwamba Yesu ni Bwana. **1 Kor.12:3** ***"Hakuna anenaye kwamba Yesu ni Bwana ispokuwa katika Roho Mtakatifu."*** Ni maksudi ya Mungu kwamba tuzaliwe mara ya pili kwa njia ya Roho.

Tunamwabudu Mungu katika Roho (**Fil.3:3**). ***"Mungu ni Roho, imewapasa wamwabuduo wamwabudu katika Roho na Kweli."*** **Yoh.4:24**

Nini inatendeka tunapozaliwa mara ya pili kwa Roho?
Punde tunapozaliwa mara ya pili **asili yetu ya ubinadamu** inaanza kutakaswa – mwili, nafsi na roho (**1 Thess.5:23**) na ***"kuhifadhiwa bila lawama".*** Awali tulikuwa wafu kwa Mungu kwa sababu ya dhambi, sasa tumehuishwa. Pale ambapo tulikuwa tumekufa kwa ajili ya dhambi, sasa tumehuishwa kwa sababu ya haki. (**Efe.2:2**)
Efe.2:4-5 ***"Bali Mungu .... hata wakati ule tulipokuwa wafu katika makosa yetu, alituhuisha pamoja na Kristo (kwa njia ya neema tumeokolewa)."***
Rum. 6:23 ***"Maana mshahara wa dhambi ni mauti, bali karama ya Mungu ya bure ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu."***
Rum. 6:11 ***"Vivyo hivyo ninyi nanyi pia, jihesabuni kuwa wafu kwa dhambi, na walio hai kwa Mungu katika Kristo Yesu Bwana wetu."***

Kwa njia ya imani katika Kristo Yesu, tunazaliwa mara ya pili kwa njia ya Roho anayetukumbusha na kutufundisha mambo yote. (**Yoh 14:26**)
Upako wa Roho ni kwa ajili ya kazi (**1 Yoh 2:20,27**) na yatupasa***"kuchochea kipawa cha Mungu"*** kilichomo ndani yetu (**2 Tim.1:6**); maana ***".tumezaliwa mara ya pili, si kwa mbegu iharibikayo bali kwa hiyo isiyoharibika kwa Neno la Mungu lenye uzima, linalodumu hata milele***." (**1 Pet.1:23**)

TUMEOKOLEWA KWA IMANI, KWA DAMU NA KWA NJIA YA ROHO
Tumeokolewa kwa njia ya imani. Imani yetu hukua kwa njia ya kuamini Neno la Mungu; kwa njia ya kusikia na kutii Neno la Mungu.
Umeokolewa kwa njia ya damu ya Yesu Kristo iliyomwagika Kalvari kuondoa dhambi za ulimwengu na iliwekwa kwenye Kiti cha Rehema juu kama upatanisho wa dhambi.

Roho Mtakatifu anahudumu na kushawishi dhambi maishani mwetu na kumfunua Yesu Kristo Mwokozi kwetu.

Tunazaliwa mara ya pili kwa njia ya Roho wakati tunapomwamini Yesu, tukiukubali msamaha wa dhambi zetu kupitia kwa damu Yake na kumpokea katika maisha yetu kama Bwana.

SURA YA PILI
NENO LA MUNGU

UTANGULIZI

Lu. 6:46-49 ***"Lakini mbona mwaniita, "Bwana Bwana", walakini hamyatendi nisemayo? Kila mtu ajaye kwangu na kuyasikia maneno yangu na kuyatenda nitawaonyesha mfano wake. Mfano wake ni mtu ajengaye nyumba na kuchimbachini sana na kuweka msingi juu ya Mwamba na kulipokuja gharika na mafuriko uliishukia hiyo nyumba kwa nguvu isiweze kuitikisa kwa kuwa imejengwa vizuri. Lakini kwa Yule alisikia ila hakutenda, mfano wake ni mtu ajengaye juu ya mchanga pasipokuwa na msingi, gharika na mafuriko yakaishukia kwa nguvu, ikaanguka mara na maangamizi yake ile nyumba yakawa makubwa."***

Haitoshi kusikia Neno. **Tulisikie Neno na tulitende! Yakobo 1:22**

NENO LA MUNGU KATIKA MWANZO

Neno la Mungu ni la uumbaji.

Mwa.1:3 ***" Kisha Mungu akasema...".*** na katika **aya ya 6, 9, 11, 14, 20, 24, 26**.

"Mungu akasema" ni neon la Mungu linafanya kazi – Yesu akiumba vitu vyote **Yoh.1:3**.

Neno la Mungu ni la uumbaji: **Ebr.11:3** ***"kwa imani twafahamu kwamba ulimwengu uliumbwa kwa Neno la Mungu hata vitu vinavyoonekana."*** **Zab.33:6** ***"Kwa Neno la BWANA mbingu zilifanyika."***

Tutii Neno la Mungu

Mwa.2:16-17 Mungu anamwamuru mwanadamu asile kutoka kwa mti wa kujua mema na mabaya.

Kutii Neno Lke kunaleta uzima; kuasi kunaleta mauti.

a.18 Mungu anafunua kujishghulisha Kwake juu ya mwanadamu.

Mwa.3:1-5 Mjaribu anapanda mbegu za mashaka katika nia ya Hawa kuhusu kuamini Neno la Mungu.

Mashaka huleta uasi na kutenganishwa na Mungu, nah ii huleta kifo cha kiroho.

Neon la Mungu ni la unabii

Mwa.3:14-19 Amri za Mungu za kiunabii, ziletazo hukumu ya kiunabii. Kila Neno la Mungu hakika litakuja kutimia. **a.15** ni ya muhimu sana. Timizo la aya hii ni nini?

Mwa.6:13 -21 Neno la Bwana lilimjia Nuhu, ***"na Mungu akamwambia Nuhu"***; neon la Mungu kwa Nuhu lilikuwa la kiunabii, likimwambia kile ambacho kitatendeka.

Neon la Mungu huleta imani

Mwa.15:1, 4-6 ***"Neno la BWANA likamjia Abramu."***

a.6 Abramu aliamini Neno la Mungu, ***"na akahesabiwa haki."***

"Imani huja kwa kusikia na kwa kusikia Neno la Mungu" **Rum.10:17**.

YESU NI NENO

Neno katika maandiko ya Kiyunani ni *logos*. Yesu ni ***Logos*** [Neno] lililohai; Biblia ni ***logos*** iliyoandikwa; Roho Mtakatifu hutamka ***logos*** ya kuongea.

Yoh.1:1-5 Yesu ni Neno la Mungu

a.14 He, ***"Neno akafanyika mwili, akakaa kwetu".***

a.16-17 Neno linaloishi lilileta Neema na kweli na ukamilifu Wake wote.

a.29 Yesu anafunuliwa kama Mwana Kondoo wa Mungu achukuwaye dhambi za dunia.

1Yoh.1:1-3 Yeye ni Neno la Uzima

Je! Wamjua Yesu, Neno la uzima? Je! Umeona na kushuhudia uwezo Wake? Je! Unawatangazia wengine kile ambacho umeona na kusikia?

MBEGU YA NENO

Yesu ni "mbegu" iliyonenwa katika **Mwa. 3:15** na kuahidiwa Ibrahimu katika **Mwa.15:3**.
Katika **Matt.13:3-9** tunasoma mfano wa Mpanzi na mbegu. Mungu anataka tujue na tufahamu siri za ufalme wa mbinguni. Anataka tusome Neno Lake na tulielewe, tuwe na macho ya kuona na sikio la kusikia. **Matt.13:18-23** inatoa ufafanusi wa mfano huo. Neno ni Injili ya Bwana wetu Yesu Kristo. Inapandwa kama **mbegu** katika mchanga aina mbali mbali, kuwakilisha mioyo ya wanadamu. Nini inaendelea ni hilo neno ndani ya moyo wako? Inaitikiaje **mbegu** ya Neno la Mungu lililopandwa mioyoni mwetu?

Tumezaliwa mara ya pili, ***"sio kwa mbegu iharibikayo bali kwa mbegu isiyoharibika, kwa njia ya Neno la Mungu linaloishi na kudumu hata milele."*** **1Pet.1:23**
a.25 ***" bali neon la Mungu ladumu hata milele. Na hili ndilo Neno la Injili tulilowahubiri."***
Rum.10:8 ***"Neno li karibu nawe, kinywani mwako na moyoni mwako, yaani Neno la imani tuihubiriyo."***

MAZIWA YA NENO

Mungu anataka tule Neno Lake. Wakristo wachanga wanahitaji maziwa ya Neno. inatupasa ***"kuyatamani mziwa ya Neno, ili tukue kwalo"*** [kukua katika wokovu] **1Pet.2:2**.
Ebr.5:12-6:2 inatupasa tujue **kanuni za kwanza** za mafundisho ya Mungu kulingana na **Ebr.6:1-2**. Hizi ni 'kanuni za kwanza' hii inamaanisha ni za msingina muhimu katika maisha ya kila Mkristo.
Efe.4:13-15 inatuhimiza ***"Kukua katika mambo yote"*** katika ***"kumfahamu Mwana wa Mungu … hata tufikie cheo cha kipimo cha utimilifu wa Kristo."***
2Pet.1:5-8 Yatupasa **tukue katika maarifa**, ili ***"tusiwe tasa wala wasiozaa katika maarifa ya Bwana wetu Yesu Kristo."***
Sio makusudi ya Mungu tuendelee kuwa watoto wachanga wanaohitaji kulishwa kwa maziwa. Inatupasa kuingia katika chakula kigumu cha Neno na tuendelee kuufikia utimilifu. Kwa hivyo tunaomba ***"kwamba Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa utukufu, awape roho wa hekima na ufunuo katika kumjua Yeye."*** **Efe.1:17**

CHAKULA KIGUMU CHA NENO

Ebr.5:14 ***"bali chakula kigumu ni cha watu wazima, ambao kwa uzoefu wa akili zao wanapambanua mema na mabaya."***
Katika **Matt.4:4** tunaambiwa kwamba, ***"Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu."*** **Tunapokea uzima** wakati tunapolipokea neon la Mungu. **Yoh.6:63** Yesu anasema ***"maneno niwaambiayo ni Roho tena ni uzima."***
Yoh.4:34 Yesu anatambua kwamba kuyafanya mapenzi ya Mungu ni **Nyama** Kwake. Tunajulishwa mapenzi ya Mungu wakati nia zetu zinapofanywa upya (**Rum.12:2**).
Yoh.6:53-58 Yesu ananena juu ya **kula mwili Wake na kunywa damu ya Mwana wa Mungu** ndio kuwa na uzima wa milele. Hili lilikuwa Neno gumu ***"kutoka wakati huo, wengi wa wanafunzi wake walirudi nyuma na hawakuenda naye tena."*** **(6:66**). Walisema ***"huu msemo ni mgumu; ni nani awezaye kuufahamu?"*** **a.50**.

Nyama ya Neno la Mungu ni Neno la haki, Ebr.5:13. Watu wengi wa Mungu hupokea tu maziwa ya Neno. Lengo la Mungu ni kwamba watu wakue waufikie utimilifu. Omba Mungu njaa ya Neno Lake na ujitolee kuwa mwanafunzi wa bidii wa Neno. **2Tim.2:15** ***"Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiyekuwa na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali Neno la kweli."***

NENO:

Li hai

Ebr.4:12 ***"Maana Neno la Mungu li hai, tena lina nguvu kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na Roho na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo."***

Lina nguvu

Yoh.1:12 *"Bali wote waliompokea, aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, wale waliaminilo Jina lake."*

1Kor.2:4 ***"Na Neno langu na kuhubiri kwangu haukukuwa kwa maneno ya hekima ya akili za wanadamu bali kwa dalili za Roho na nguvu Zake.***

1Kor.4:20 ***"Maana ufalme wa Mungu hauwi kwa Neno tu bali kwa nguvu."***

Linatakasa

Eph.5:26 Kristo alilipenda kanisa hata akajitola kwa ajili yake, ***"ili maksudi alitakase na kulisafisha kwa maji ya neno."***

Linaosha

Yoh.15:3 ***"Ninyi mmekwisha kuwa safi kwa sababu ya lile Neno nililowaambia ninyi."***

Huweka safi

Zab.12:6 ***"Maneno ya Mungu ni maneno safi, kama fedha iliyojaribiwa na iliyosafishwa mara saba."***

Linakua kwa nguvu na linashinda **Matendo19:20**

Kwa sababu neno la Mungu lilikua kwa njia kuu na kushinda, ***"Hata wote waliokaa wakalisikia Neno la Bwana Yesu, Wayahudi kwa Wayunani."*** **Matendo 19:10**

Linadumu milele

Mk. 13:31 ***"mbingu na nchi zitapita lakini maneno yangu hayatapita."***

Humfunua Bwana

1 Sam.3:21 ***"Naye Bwana akaonekana tena huko Shilo, kwa kuwa Bwana akajifunua kwa Samweli huko Shilo kwa Neno la Bwana."***

Husababisha imani kukua

Rum.10:17 ***"Imani huja kwa kusikia, na kusikia kwa Neno la Mungu."***

Hufunua mapenzi ya Mungu

Matt.28:20 ***"Na kuwafundisha kushika yote niliyowaamuru ninyi."***

Yoh.7:16-17 ***"Mtu akipenda kuyatenda mapenzi yake atajua habari ya yale mafunzo, kwamba yatoka kwa Mungu ama kwamba mimi nanena kwa nafsi yangu tu."***

Yoh.15:7 ***"mkikaa ndani yangu, na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa."***

MAANDIKO YOTE NI PUMZI YA MUNGU

Biblia haijabeba tu Neno la Mungu; ni Neno la Mungu.

2 Tim.3:16 ***"Kila andiko lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kw kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki."*** Lina pumzi ya Mungu; liliandikwa kwa kusudi.

Rum.15:4 ***"Kwa kuwa yote yaliyotangulia kuandikwa, yaliandikwa ili kutufundisha sisi ili kwa saburi na faraja ya maandiko tupate kuwa na tumaini."***

Ni **Neno la hakika la unabii** ambalo ***"halikuja kwa mapenzi ya mwanadamu, bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu."***
2 Pet.1:20-21

Linamfunua Yesu Kristo. Lu. 24:27

KUFUNDISHWA KATIKA NENO.
Roho Mtakatifu ni mwalimu wetu:
Isa.30:20-21 ***"Na ingawa Bwana atawapeni chakula cha shida na maji ya msiba, lakini waalimu wako hawatawaficha tena ila macho yako yatawaona waalimu wako na masikio yako yatasikia Neno nyuma yako likisema, "Njia ni hii ifuateni" mgeukapo kwenda mkono wa kuli na mgeukapo kwenda mkono wa kushoto.'"***

Yoh.14:26 ***"Lakini huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu ambaye Baba atampeleka kwa jina langu atawafundisha yote na kuwakumbusha yote niliyowaambia."***
Yoh.16:13 ***"Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa Kweli atawaongoza awatie katika kweli yote atakayoyasikia atayanena."***

Kufundisha ni kipawa:
Rum.12:6-7 kufundisha, kipawa kulingana na neema ya Mungu.
1 Kor.12:28 Mungu ndiya aliyewaweka wengine kuwa waalimu kanisani.
Efe.4:7-11 Mwalimu ni mmoja kati ya karama ambazo Yesu alitoa .
Yakobo 3:1 Ametoa onyo maalum kwa Waalimu.

***Kila muumini anapaswa kukua awe mwalimu*:**
Ebr.5:12 - 6:2 Waumini wote wanatakikana kufundishwa ili waweze kufundisha wengine misingi ya imani.
1 Pet.4:11 Inatupasa kunena maneno ambayo Mungu anatupatia kunena, ***"Kama kusema maneno ya Mungu."***

Wazee lazima waweze kufundisha:
Tito 1:9 ***"Akilishika lile Neno la imani vile vile kama alivyofundishwa apate kuweza kuwaonya watu kwa mafundisho yenye uzima na kuwashinda wenye kupinga."***
1 Tim.3:2 Wazee wanatakikana kujua kufundisha Neno.

Kua Katika Mambo Yote Katika Yeye:
Efe. 4:11-16 lengo la kufundisha ni kuleta kanisa katika ukamilifu.

Upako waliopewa waalimu:
1Yoh. 2:20 ***"Nanyi mmepakwa mafuta na Yeye aliye Mtakatifu nanyi mnajua yote."***
:27 ***"Nanyi mafuta yale mliyoyapata yana kaa ndani yenu wala hamna haja ya mtu kuwafundisha lakini kama mafuta yake yanavyowafundisha habari za mambo yote tena ni kweli wala si uongo na kama yalivyowafundisha kaeni ndani yake."***

Upako wa Roho Mtakatifu katika maisha yetu hutufundisha
Omba Roho Mtakatifu: atakushawishi, fundisha na kukufunulia mambo yote.

SURA YA TATU
ROHO MTAKATIFU NI NANI?

Yoh. 7:37-39 ***"Hata siku ya mwisho, siku ile kubwa ya sikukuu, Yesu akasimama , akapasa sauti yake akisema, 'mtu akiona kiu na aje kwangu anywe. Aniaminiye mimi kama vile maandiko yanavyosema, mito ya maji yaliyohai yatatoka ndani mwake. Na Neno hilo alisema katika habari za Roho Mtakatifu, ambaye wamwaminio, watampokea baadaye kwa maana Roho Mtakatifu alikuwa hajaja kwa sababu Yesu alikuwa bado hajatukuzwa."***

Katika andiko hili Yesu anathibitisha na kuendeleza kuashiria kwa agano la kale kuwa maji ya mito [mvua] na huduma ya Roho Mtakatifu katika maisha ya watu.

AHADI YA BABA

Katika **Matendo 1:4** Yesu aliwaambia wangojee ***"ahadi ya Baba"***: Baba alikuwa ameahidi Roho Mtakatifu.

Lu. 24:49 ***"Tazama, nawaletea juu yenu ahadi ya Baba Yangu, lakini kaeni humu mjini hata mvikwe na uwezo utokao juu."***

Yoh. 14:26 ***"Lakini huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu atawafundisha yote na kuwakumbusha yote niliyowaambia."***

Roho Mtakatifu ni Ahadi ya Baba.

Maandiko Fulani katika Agano la Kale ambayo yanaahadi ya Roho Mtakatifu:

Yoeli 2:28 Mungu anasema ***"siku za mwisho, Nitamwaga Roho yangu juu ya wote wenye mwili."***

Katika **Matendo 2:17-21** Petro ananakili Yoeli. Petro anasema nini katika **Matendo 2:16**? ***"Lakini jambo hili ni lile lililonenwa nakinywa cha nabii Yoeli."***

Ezek.36:26-27 ***"nami nitawapaninyi moyo mpya, nami nitatia roho mpya ndani mwenu, nami nitatoa moyo wa jiwe uliomo ndani ya mwili wenu, nami nitawapa moyo wa nyama. Nami nitaia roho yangu ndani mwenu na kuwaendesha katika sheria zangu nanyi mtazishika hukumu zangu na kuzitenda."***

Jer.31:31-34 Inaashiria Agano Jipya. Mungu ataziandika sheria zake juu ya mioyo yetu na katika nia zetu. Mungu anafanya haya kwa kumtuma Roho Mtakatifu akadumu ndani mwetu punde tu tunapompokea Yesu. Hii mistari imenakiliwa katika **Ebr. 8:8-12**, **10:16**.

Zek.4:6 ***"Sio kwa nguvu wala kwa uwezo, bali kwa Roho Wangu."*** 'Nguvu' na 'Uwezo' maana yake ni nini? 'Nguvu' inaashiria nguvu za mwanadamu, san asana kama nguvu za kijeshi; 'Uwezo' unaashiria uwezo wa mwanadamu.

Isa.43:19b Ahadi ya ***"mito ya maji jangwani."*** Linganisha hili na **Yoh.7:38**.

Isa.12:3 ***"Basi kwa furaha mtateka maji katika visima vya wokovu"***, inaongea kuhusu maji yaliyo hai.

ROHO MTAKATIFU ULIMWENGUNI

Roho Mtakatifu alihusika katika uumbaji, **Mwa.1:2** ***"Nchi ilikuwa ukiwa tena utupu na giza lilitanda juu ya uso wa vilindi vya maji; Roho ya Mungu ikatulia juu ya uso wa maji."***

Roho Mtakatifu alifanya kazi duniani katika nyakati kabla ya kuja kwa Yesu; lakini inaonekana hakuwa amefunuliwa kikamilifu wala hangeweza kuleta makusudi ya Mungu kutimia hadi wakati Mwana wa Mungu atakapokuja kuleta ukombozi duniani. Alikuwa hajadhihirika katika ukamilifu wa njia Mungu alivyokuwa amekusudia maana wakati ulikuwa haujawadia. Kutoka kwa **Yoh.7:39** tunajua **hangekuja hadi Yesu atukuzwe.**

Tukiangalia mifano kadhaa katika Agano la Kale, tunaona kazi ya Mungu Roho Mtakatifu kabla ya kuja kwa Yesu:

Waam.14:6, kuhusu Samsoni, ***"Roho ya Bwana ikamjia kwa nguvu naye akampasua kana kwamba anampasua mbuzi,*** na aya ya**.19** ***"Roho wa BWANA akamjia kwa nguvu, naye... akawauwa wa thelathni."***

Waam.6:34 ***"Lakini Roho ya BWANA ikaja juu ya Gideoni: akapiga tarumbeta."***
Roho Mtakatifu ***"alikuja juu"*** **ya watu hawa na kuwatia nguvu** kutenda matendo makuu, akiwapa nguvu na ujasiri ambao kibinadamu hawakuwa nao.
Yesu alipokuja , alisema kutakuwa na ***"mito yabubujikiayo kutoka ndani yao,"*****Yoh.7:38**.
Roho Mtakatifu angekuja ndani ya kila muumini, kumpa nguvu na ujasiri usiokuwa wa kawaida. Tambua tofauti: katika Agano la Kale, Roho Mtakatifu alikuja juu ya watu Fulani waliochaguliwa ili kuwawezesha kutenda matendo ya Mungu; katika Agano Jipya Roho Mtakatifu anakaa ndani ya kila muumini kumuwezesha kila muumini kuwa Nabii, Kuhani na Mfalme!

YESU NA ROHO MTAKATIFU
Yohana alimtambua Yesu kupitia kwa kuja na kujidhihirisha kwa Roho Mtakatifu.**Yoh.1:32-34**. Baba alikuwa amemjulisha Yohana kile cha kuangalia, **a.33** ***"Yeye ambaye utamwona Roho akishukana kukaa juu yake , huyo ndiye abatzaye kwa Roho Mtakatifu."***

Yoh.3:34 Yesu alipokea Roho Mtakatifu***"bila kipimo"***.
Ebr.1:9b ***"Kwa hivyo, Mungu, Mungu wako amekutia mafuta. Mafuta ya shangwe kupita wenzio."*** Mwandishi ananakili kutoka **Zab.45:7**. **Zaburi 45** ni Zaburi ya kimasihi inayonena kuhusu Yesu na kanisa Lake.

Yesu alituwekea mfano wa kufwata: ubatizo wa maji na kujazwa na Roho **Matt.3:13-17**. "Ubatizo' Wake ulikuwa chanzo cha huduma yake wazi:
Lu.4:1 Yesu aliongozwa na Roho kwenda nyika kujaribiwa na shetani;
Lu.4:14 Yesu alirudi kutoka jangwani katika nguvu za Roho Mtakatifu;
Lu.4:18 Yesu anatangaza na kuweka wazi huduma yake – ***"Roho wa Bwana yu juu yangu, kwa maana amenitia mafuta …"***
Yesu hakuanza huduma wazi kabla ya kujazwa na kutiwa nguvu na Roho Mtakatifu.

YESU ALIONGEA KUHUSU KUJA KWA ROHO MTAKATIFU NA HUDUMA YAKE
Yoh.14:16 ***"Nami nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine ili ake nayi hata milele."****Neno la Kiyunani la 'Msaidizi' ni 'parakletos' SC.#3875: Neno hilo linaashiria mwombezi, mfariji, msaidizi, wakili, Mshauri. Katika uandishi usikuwa wa Biblia 'parakletos' ilikuwa na maana ya Yule mtu anayewakilisha mwingine katika mahakama. Roho Mtakatifu anamwongoza mtu katika kuelewa zaidi ukweli wa Injili. Kuongezea kwa kusaidia na kuongoza, anapeana nguvu za kustahimili ukatili wa sera za kidunia . (Word Wealth, Spirit Filled Life Bible, p.1605)*
Yoh.14:17 Yeye ni Roho wa kweli, ambaye ulimwengu hauwezi kupokea, ***"lakini ninyi mwamjua, maana anakaa kwenu na atakuwa nanyi."***
Yoh.14:26 Anatumwa na Baba na ni Msaidizi wetu, Mwalimu Na Yule ambaye ***"atawakumbusha mambo yote niliyowaambia ninyi."***
Yoh.15:26 Yeye ni Roho atokaye kwa Baba na anamshuhudia Yesu.
Yoh.16:7 Hangeweza kuja hadi Yesu aliporejea mbinguni, ***"Yafaa ninyi mimi niondoke, kwa maana nisipoondoka, huyo Msaidizi hatakuja kwenu, bali mimi nikienda zangu, nitampeleka kwenu."***
Yoh.16:8-11 Yeye ni Roho ambaye ataushawishi ulimwengu kuhusu dhambi na kuhusu haki na kuhusu hukumu.
Yoh.16:13 Yeye ni Roho ***"atakaye waongoza katika kweli yote; kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe lakini yote atakayoyasikia atayanena na mambo yajayo atawapasha habari yake."***

Yoh.16:14 Roho Mtakatifu atamtukuza Yesu kila mara ***"kwa kuwa atatoa yaliyo yangu na kuwapasha habari."***
Yoh.16:15 ***"Yote aliyonayo Baba ni yangu, kwa hivyo nalisema ya kwamba atatwaa kwa yaliyo yangu na na kuwapasheni habari."***
Roho Mtakatifu ameshuka kutoka kwa Baba na Mwana ili kumfanya Mungu ajulikane kwetu na kunena Neno Lake ndani mwetu.

AGANO JIPYA
Mungu alikuwa na mpango wa kurejesha mwanadamu kwake Mwenyewe; kwa njia ya kuzaliwa mara ya pili kwa Roho Mtakatifu (**Yoh.3:5-6**), Anayatuleta katika ushirika na Mungu. Mungu aliahidi kupita kwa manabii kwamba atafanya Agano Jipya na watu wote. Agano Jipya ni **'katika Roho**. ***"Mungu ni Roho na wamwabuduo imewapasa kumwabudu katika Roho na kweli."*** **Yoh.4:24**. Kupitia kwa Agano Jipya, Mungu atafunuliwa kwa watu Wake katika njia ambayo watakatifu wa Agano la Kale waliona tu katika maono na unabii.

Mwanadamu alianguka katika mwili, uadui na Mungu
Roho ndiye suluhisho la maatizo ya mwanadamu.
Gal.5:16 ***"Enendeni katika Roho wala hamtazitimiza tena tamaa za mwili."***
a.17 ***"Kwa maana mwili hutamani ukashndana na Roho na Roho kushindana na mwili kwa maana hizi zinapingana."***
a.18 ***"Lakini mkiongozwa kwa Roho, hampo jinni ya sheria."***
a.19-21 Inaorodhesha matando ya mwili.
a.21b ***"watu wanaoyatenda mambo kama hayo hawataurithi ufalme wa Mungu."***
Tuna hitaji Roho Mtakatifu ndani yetu ili atufundishe Neno la Mungu na Kunenea katika mioyo yetu na nia zetu. Bila Yeye ni vigumu kuushinda ulimwengu.

Agano Jipya liko katika Roho
Mungu aliahidi Roho watu Wake (**Ezek.36:26-27**) na kuahidi ***agano bora***, Agano Jipya ambapo Roho Atakuja na kukaa na watu ndani ya watu wa Mungu. Ilibidi Mwokozi afe ili aweze kuwakomboa wanadamu, damu yake inatuosha kutoka kwa kila dhambi, ili tuweze kupokea Roho wa Mungu. Tunapoitikia Injili tunapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. **Matendo 2:38** ***"Tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, na mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."*** **Hiyo ndiyo ahadi!** Na ahadi ni "***kwenu na watoto wenu na wote walio mbali."***

Hatuwezi kupkea Roho wa Mungu katika maisha yetu hadi tutakapotubu **dhambi** na kupokea **msamaha** wa dhambi kwa njia ya kufa kwa Yesu Kristo msalabani. Katika **Matendo 19:1-6**, wanafunzi ambao Paulo alipata Efeso walikuwa bado hawajasikia injili – walikuwa wamapokea tu mafundisho ya Yohana Mbatizaji. Iliwabidi kumwamini Bwana Yesu na kubatizwa katika Jina Lake ndipo wapokee Roho Mtakatifu. Tambua kwamba iliwabidi kubatizwa tena maana ubatizo wa kikristo una maana tu kwa sababu ya msalaba – umwagikaji wa damu – na ubatizo wa Yohana haukutoshana na ubatizo wa Kikristo.

ROHO MTAKATIFU - MTU
Yesu alinena kuhusu Roho kama Mtu, Mwalimu, Anayeelekeza, Mfariji, Roho wa kweli katika **Yoh. Sura.14-16.**

Uhusiano wetu Naye
Roho Mtakatifu anaweza **kuhuzunishwa**. Huzuni ni hisia ya ndani. Paulo anamfanya Roho kuwa Mtu katika **Efe.4:30** ***"Wala msimhuzunishe huyo Roho Mtakatifu wa Mungu ambaye kwa yeye mlitiwa muhuri katika siku ya ukombozi."***

Tumepewa Roho Mtakatifu kama **chapa ya *ukombozi wetu*** (**Efe.1:13**) kuashiriakumilikiwa na Mungu – tumenunuliwa kwa bei.

Roho Mtakatifu anatujali na ***hututakasa*** sisi (**Rum.15:16**).

Tunaweza kuwa na ***ushirika*** na Roho Mtakatifu (**2 Kor.13-14**): tunaweza kushiriki, kunena na kupokea kutoka kwa Roho Mtakatifu na kufurahia Uwepo Wake katika maisha yetu .

Roho Mtakatifu anaweza **Kuzimwa**. Tukikatiza yale ambayo Roho anatupatia kama watu binafsi ama kundi, ***"Tunamzima Yeye."*** **1Thess.5:19** Ni muhimu tukue tukiwa waangalifu kwa mwelekeo na msukumo wa Roho Mtakatifu, tukidhamini kipawa cha upako katika maisha yetu na kujifunza mtiririko wa Roho katika mikutano yetu.

Tunajengwa na ***kuwezeshwa*** na Roho Mtakatifu kuwa watumishi wa Agano Jipya.
2 Kor.3:3-6 Ninyi ni waraka wake Kristo; ulioandikwa kwa Roho wa Mungu Aishiye;
Sio katika vibao vya mawe bali katika mioyo;
Utoshelevu wet uni kutoka kwa Mungu: Amwtufanya kuwa wahudumu wa Agano Jipya katika Roho. Roho anapeana uzima.

Tunaweza tu kuomba kikamilifu kwa **[katika] Roho**; ***"Kwa sala zote na maombi mkisali kila wakati katika Roho."*** **Efe.6:18**
Ni kwa njia ya Roho tunaabudu, ***"tukibadilishwa katika mfano wa sura yake kutoka utukufu hadi utukufu utokao kwa Bwana kwa Roho."*** **2 Kor.3:18**

Mungu anatamani tuwe na Roho ndani yetu, ili tuishi na kuenda katika Roho (**Gal.5:25**). Bila yeye, hatuwezi kuishi maisha ya Kikristo. Tukiwa Naye tunaweza kufurahia **Tunda Lake** katika maisha yetu: upendo, furaha, amani, uvumilifu, utu, wema, fadhili, uaminifu na kiasi. (**Gal.5:22-23**)

Dhambi isyosamehewa.
"Kila dhambi na neno la kufuru watasamehewa wanadamu [hiyo ni kufuru kuhusu Mungu na Mwana] ***bali kumkufuru Roho Mtakatifu hawatasamehewa. Naya yeyote atakayenena neno juu ya Mwana wa Adamu atasamehewa bali yeye atakaye nena juu ya Roho Mtakatifu katika ulimwengu wa sasa walaa katika ujao."***
Yesu alinena mambo hayo katika mkutadha wa mafarisayo wakisema kwamba alitenda miujiza na kutoa Pepo ***"kwa Beelzebubu, mkuu wa mapepo,"*** **Matt.11:24**. Kunahitajika kuwa na upambanuzi kati ya nguvu za shetani na nguvu za Roho wa Mungu. Tukirudi Mwanzo, Adamu alikatazwa na Mungu ***"kula matunda kutoka kwa mti wa kujua mema na mabaya"*** **Mwa.2:7**. Mwanadamu aliacha kula kutoka kwa Mti wa Uzima baada ya kudanganywa na shetani. Hata sasa bado kuna kuchanganyikiwa kuhusu ilimwengu wa kiroho na mara nyingi wanaoitwa Wakristo wamenena kinyume na nguvu za vipawa vya Roho wakisema ni nguvu za shetani.

Ishara nyingi na maajabu yanaweza kutendeka katika nguvu za shetani (**Ufu.13:13**). Tunahitaji kujua ***"sisi ni wa Roho gani"*** na inawezekana kwa Roho Mtakatifu, tukiishi ndani Yake na kutembea kwa neema Yake na nguvu Zake.

Mungu anataka zaidi tuishi na kuongozwa na Roho
Na uje Roho Mtakatifu
Umekaribishwa ndani ya maisha yangu
Nina kuhitaji!
Siwezi kufanya lo lote bila Wewe
Jinsi tunavyompokea Yesu kama Mwana wa Mungu ndani ya maisha yetu kwa imani, kuamini Neno Lake,Ndivyo tunampokea Roho Mtakatifu maishani kwa imani kulingana na Neno Lake.

SURA YA NNE
ROHO MTAKATIFU ANAKUJA
JINSI YA KUJAZWA

Kabla ya Yesu kupaa, aliwapa wanafunzi Wake ahadi, **Lu.24:49** ***"Tazama, nawaletea juu yenu ahadi ya Baba Yangu; lakini kaeni humu mjini hadi mvikwe nguvu zitokazo juu."*** Katika **Matendo 1:4** Yesu aliwaambia waingojee ahadi ya Baba. Katika **Matendo 1:5** Akawaambia ***"mtabatizwa na Roho Mtakatifu baada ya siku hizi chache."*** Na tena katika **Matendo 1:8** ***"mtapokea nguvu akiisha kwachilia Roho Mtakatifu juu yenu."***

Yesu aliwaambia wanafunzi Wake watarajie kujazwa na Roho Mtakatifu;
Watapokea nguvu.
Ahadi ya Baba ni Roho Mtakatifu.

Katika **Matendo 2** tunaona kutimia kwa ahadi hiyo.

ROHO MTAKATIFU ALIKUJA VIPI?

Roho Mtakatifu alikuja Siku ya Pentekoste.
Alishuka kwa nguvu, ishara za ajabu na vipawa.

Matendo 2:2-8 sauti kama upepo mkuu, ndimi za moto, ***wakajazwa na Roho Mtakatifu, na kuanza kenena kwa lugha mpya.…"***.
Kujithihirisha kwa kwanza katika wanafunzi kulikuwa katika 'kunena kwa lugha mpya.]'.
Maten. 2:6 ***"… kila mtu aliwasikia wakinena kwa lugha yake mwenyewe …"***
Maten. 2:11 ***"wakisema kwa lugha zetu matendo makuu ya Mungu."***

Wanafunzi walikuwa wakinena katika lugha za wanadamu. Kulikuwa na makundi ***kumi na sita*** tofauti ile siku, na walisikia injili ikihubiriwa katika lugha yao wenyewe. Baada ya kujazwa na Roho Mtakatifu, Petro aliweza kuhubiri kwa ujasiri habari za Yesu. Petro alitoa taarifa kuu ya Yesu kama mtu ***"aliyethihirishwa kwenu kwa ishara na maajabu"***, akasulubiwa na kufufuka; kasha akanena juu ya Bwana Aliyepaa anaye kaa katika hukumu. Aliwambia kwamba ***"na nyumba yote ya Israeli wajue kwa hakika ya kwamba Mungu amemfanya huyo Yesu kuwa Kristo na Bwana."*** **a.36**

Matendo 2:37 wasikilizaji walishawishiwa na Neno lililojawana Roho Mtakatifu. Waliolipokea Neno walibatizwa (**a.41**). ***"Kila mtu akajawa na hofu; ajabu nyingi na ishara zikafanyika kwa mikono ya mitume ."*** **a.43**
Matokeo ya kushuka kwa Roho: ***ishara na maajabu***.

WANAFUNZI WALIOKOKA LINI?
Yesu anatwambia katika **Yoh.3:3-6** ya Kwamba ni lazima tuzaliwe kwa Roho. Roho Mtakatifu hangeweza kukaa ndani ya mtu kabla ya Yesu kuteswa na kufa msalabani na kuchukuwa dhambi zetu. Kwa hivyo twauliza swali: wanafunzi waliokoka lini? Tunajua kwamba walipokea Roho Mtakatifu na Nguvu Siku ya Pentekoste. Lakini baada ya kufufuka katika **Yoh.20:22** Yesu alikuja kwa wanafunzi ***"Akawavuvia akawaambia, 'Pokea Roho Mtakatifu'"***. Kwa sababu Yesu alikuwa ametoka msalabani na wanafunzi walikuwa wamemwamini katika ufufo Wake, waliwezeshwa kupokea Roho katika mtu wa ndani yao.

Je! Umezaliwa mara ya pili kwa Roho? Hii ni hatua ya kwanza: kumpokea Kristo kwa Roho katika mtu wa ndani. Halafu utaweza kujazwa ama kutiwa nguvu na Roho. Kuzaliwa mara ya pili na kujazwa roho mtakatifu ni mambo mawili tofauti ambayo ni ya msingi katika kumjia Yesu Kristo.

NITAWEZAJE KUMPOKEA ROHO MTAKATIFU?

1. ***Kwa kuomba***. **Lu.11:13** ***"Basi ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vilivyo vyema, je, Baba wa mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu wale wamwombao!"*** Baba wa mbinguni Anaahidi kutupatia Roho Mtakatifu.
2. ***Kwa kutii amri zake***. **Yoh.14:15-16** ***"Mkinipenda mimi, mtazishika amri zangu. Na nitamwomba Baba Yangu na atawapeni Msaidizi Mwingine, ili akae nanyi hata milele – Roho wa kweli."***
3. ***Kwa kkukundua kuwa tayari anakaa nasi*** **na yumo mwetu kwa njia ya imani ndani ya Yesu**. **Yoh.14:17b** ***"Bali ninyi mnamjua, maana anakaa kwenu na atakuwa ndani yenu."***
4. ***Kwa kutubu*****, Kwa kubatizwa katika Jina la Yesu kwa ajili ya msamaha wa dhambi, utapokea kipawa cha Roho Mtakatifu, Matendo 2:38**
5. ***Kwa njia ya kuwekewa mikono*** **Punde tu unapompokea na kumwamini Yesu na kubatizwa. Matendo 8:16-17** ***"Ila walikuwa wamebatizwa tu katika Jina la Bwana Yesu. Ndipo wakaweka mikono yao juu yao, na wakampokea Roho Mtakatifu."*** [pia **Matendo19:5-6**]
6. ***Kwa kuliamini Neno lililohubiriwa*** **kuhusu Yesu, Yeye Roho Mtakatifu atawajilia juu yenu. Matendo 10:44-45**.

ROHO MTAKATIFU NI KAMA NINI?

Ni ***Mtu***; Yesu Kristo alinena juu Yake kama 'Yeye' (**Yoh.14:16**).
Yeye ni kama ***Yesu*** (**Yoh.14:16**); ni Roho wa Kristo (**Rum.8:9**); Ni Mfariji (**Yoh.14:16**)
Atanena sana kuhusu Yesu, ***"Atawafundisha yote niliyowaambia, na kuwakumbusheni mambo yote."*****Yoh.14:26**. ***"Atanitukuza mimi, maana atchukua kwa yaliyo yangu na kuwajulisha ninyi."*** **Yoh.15:14**
Alidhihirishwa kama ***Huwa*** wakati wa ubatizo wa Yesu(**Matt.3:16**)
Alidhihirishwa katika ***ndimi za moto*** na sauti ya upepo mkuu (**Matendo 2:2-3**)
Uwepo wake huja katika mfano wa ***wingu la Kiungu*** (**Matt.17:5**, **Kut.40:34-38**)
Amejaa ***uweza*** na ***hutia*** hizo nguvu kwetu (**Matendo 1:8**)
Ana **uweza** mwingi wa Kiungu na hutia vipawa katika waaminio (**1 Kor.12:4-11**)
Yeye ni ***"upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili na uaminifu, kiasi, upole"***: yote yakidhihirika katika ukamilifu wa Mungu Baba (**Gal.5:22-23**).
Anaweza ***kuhuzunishwa*** (**Efe.4:30**); Uwepo wake na upako Wake unaweza kuzimwa (**1 Thess.5:19**).

YESU NDIYE ANAYEBATIZA KATKA ROHO MTAKATIFU

Yohana anaeleza kinganaga kwamba Yesu atawabatiza kwa Roho Mtakatifu.
Matt.3:11 ***"Atawabatiza kwa Roho Mtakatifu na moto."***
Mk.1:8 ***"Mimi naliwabatiza katika maji, bali Yeye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu."***
Lu.3:16 ***"Atawabatiza kwa Roho na Moto."***

Yesu pia alisema kuwa Yeye ndiye atakaye mtuma Roho Mtakatifu. **Lu.24:49** ***"Tazameni nawatumia Ahadi ya Baba Yangu juu yenu; lakini kaeni humu mjini hadi mtakapovikwa uweso utokao juu."***
Ni Baba ndiye aliyekuwa amemjulisha Yohana kwamba Yesu ndiye atakaye wabatiza katika Roho Mtakatifu. **Yoh.1:33** ***"Wala mimi sikumjua, lakini Yeye aliyenipeleka kubatiza kwa maji huyo aliniambia; Yeye ambaye utamwona Roho akishuka juu yake na kukaa juu yake, huyo ndiye abatizaye kwa Roho Mtakatifu."***

Wanjilisti wanne [Mathayo, Marko, Luka na Yohana] wote wanashuhudia ubatizo kwa Roho Mtakatifu. Kila neno linadhibitika kwa ushuhuda wa vinywa vya watu wawili ama zaidi. Injili zote nne zinadhibitisha mafundisho Fulani ya Yesu; na ubatizo ni mojawapo. Kwa hivyo ni ni muhimu na niwakipekee!

KUJAZWA NA ROHO MTAKATIFU KATIKA MATENDO – SOMO:
Ilitendekaje Siku ya Pentekoste?
Matendo 2:1-4 walikuwa ***katika umoja mahali pamoja***.
a.2 Kisha ikatokea **sauti kama ya upepo uvumao kutoka mbinguni** ,
a.3 ***Ndimi za moto zikatokea na kukalia kila mmoja wao***.
a.4 Wote ***wakajazwa*** na kuanza kunena katika lugha nyingine.
Matendo 2:6-8 ***Watu waliwasikia wanafunzi wakinena*** katika lugha zao wenyewe.

Matendo 2:17-21 ***Unabii unatimia***: Petro akatambua kwamba hili ni kulingana na unabii wa **Yoeli 2:28-32**. Baada ya kujazwa na Roho Mtakatifu, Petro aliweza kuhubiri kwa ujasiri juu ya Yesu.
Matendo 2:38 inatwambia kile ambacho wanafunzi walihitaji kufanya ili wapokee kipaw cha Roho Mtakatifu. ***"Petro akawaambia, 'Tubuni basi, na kila mmoja wenu abatizwe katika jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi; na mtapokeakipawa cha Roho Mtakatifu.'"***

Kujazwa na Roho Mtakatifu ni tukio linaloendelea
Matendo 4:8 ***"Ndipo Petro, akijawa na Roho Mtakatifu …"***
Matendo 4:31 ***"…wote wakajawa na Roho Mtakatifu wakanena Neno la Mungu kwa ujasiri."***

Huduma yenye nguvu hutokana na kujazwa Roho Mtakatifu
Matendo 6:3 ***Wasaidizi wa kwanza*** walihitajika kuwa wamejazwa na Roho Mtakatifu na hekima.

Baada ya kuokoka bado tunahitaji kipawa cha Roho Mtakatifu
Matendo 8:12 ***Wengi waliitikia injili*** iliyohubiriwa Samaria, wakaokoka na kubatizwa.
Matendo 8:14-16 lakini bado wanahitaji kujazwa, kupokea kipawa cha Roho Mtakatifu;
Matendo 8:17-18 ***Hiki kipawa walikipokea baada ya kuwekewa mikono***.
Matendo 9:17-18 ***Sauli aliponywa***, na kujazwa Roho Mtakatifu kisha akabatizwa.
Matendo 10:44-48 Hii ni habari ya kwanza ya Mataifa kupokea Roho Mtakatifu; waliamini Neno alilohubiri Petro; Roho Mtakatifu akawachilia juu yao [kama alivyo wachilia wayahudi walioamini siku ya Pentekoste], Kisha wakabatizwa katika maji.
Matendo 19:1-7 inaandika juu ya tukio la huko Efeso, amini Yesu, batizwa kwa maji [kubatizwa tena], kujazwa na Roho Mtakatifu na vipawa kuwachilia juu yao kwa njia ya kuwekewa mikono.

KUNENA KWA LUGHA MPYA

Walinena kwa lugha mpya baada ya kujazwa na Roho Mtakatifu;
Matendo 2:4 ***"Wote wakajazwa na Roho Mtakatifu na wakaanza kunena kwa lugha mpya, kama vile Roho alivyowawezesha."***
Matendo 9:17 ***"Ndugu Sauli … ujazwe na Roho Mtakatifu"***; Paulo anatangaza katika **1Kor.14:18** Paulo akisema ***"Namshukuru Mungu kwa kuwa ninanena kwa lugha zaidi ya ninyi nyote."***
Matendo 10:44-46 Kunena ama kuomba katika lugha, ama kwa lugha nyingine ambayo hukujifunza, ni thihirisho la kawaida la kujazwa na Roho Mtakatifu katika Maandiko Matakatifu. Katika nyumba ya Kornelio, Petro pamoja na waaminio wa tohara walitambua kwamba Roho Mtakatifu alikuwa amewashukia Mataifa wakati walipoanza kunena kwa lugha nyingine na kumtukuza Mungu
Matendo 19:6 ***"Na Paulo alipokwisha kuweka mikono yake juu yao, Roho Mtakatifu akaja juu yao wakaanza kunena kwa lugha na kutabiri."***

Kutimia kwa ahadi Yake
Yesu aliahidi kumtuma Roho Mtakatifu kwa wanafunzi Wake baada ya kurdi Mbinguni. Aliwaambia Baba alikuwa ameahidi (**Matendo 1:4**) Roho Mtakatifu pia. Aliwaambia wanafunzi wake kungojea Yerusalemu ***"hadi mtakapovikwa nguvu kutoka juu."*** (**Lu.24:49**) Wanafunzi [120] walijazwa [walipokea] nguvu, walibatizwa kwa Roho Mtakatifu Siku ya Pentekoste. Ishara kwa makutano waliokuwa wamekusanyika kwamba kuna kitu kipya ambacho kimetendeka, ni kwamba walikuwa wakinena kwa lugha mpya pamoja na tabia zingine kama za kulewa; walikuwa wamepokea Roho Mtakatifu katika njia ya Agano Jipya, kitu kipya kabisa ambacho Mungu alikuwa anafanya baada ya Yesu kufa, kufufuka na Kupaa juu, (**Matendo 2:4**).

Ubatizo katika Roho Mtakatifu na kunena kwa Lugha Mpya
Katika hali ya wanafunzi Siku ya Pentekoste, ndimi zilikuwa za wanadamu, ama chache yazo zilikuwa (**Matendo 2:6**). Kunena kwa lugha ambako kunanenewa katika **Matendo** ni thihirisho la **'kipawa cha kunena katika lugha'** kinachonakiliwa katika **1 Kor.12:10**. Hata, hivyo, ndimi zinapotolewa na Roho Mtakatifu kama ishara ya kubatizwa katika Roho Mtakatifu, hazihitaji kutafsiriwa. **Ishara ya Biblia**, ama **Matendo makuu ya Mungu** katika ubatizo wa Roho Mtakatifu ni **Kunena kwa lugha**. Kunena katika lugha ni kipawa[cha Kikungu] **kinapatikana kwa kila aaminiye**. Ni kipawa cha nguvu ambacho kila mwaminio anahitaji kuwa nacho kwa sababu ya maombi ya binafsi na kujijenga (**1 Kor.14:2&4**), yaani, kukua na kutiwa nguvu katika maisha ya kiroho ya mtu binafsi.

Tunapokea Roho Mtakatifu kwa imani kutoka kwa Yesu na kujitolea miili yetu na nafsi zetu Kwake. Anadhibitisha uwepo wake na nguvu kwa kuwachilia nguvu za Mungu, kipawa cha Mungu, ambacho kinamuwezesha mwamini **kunena kwa njia ya Kimungu, kwa lugha ama kutafsiri**. Kipawa kinakaa nasi, na tunatumia hicho kipawa kutumia nguvu za Roho Mtakatifu. Na hivyo, Paulo anaomba katika ndimi kuliko ninyi nyote (**1 Kor.14:18**).

Kunena katika lugha *'chrisma'* [kipawa] ambach Roho hupeana. Kipawa cha ndimi ambacho ni ishara ya kubatizwa katika Roho siku ya ubatizo kwa mwaminio. Kinapatikana kwa kila mwamini, kama sehemu ya kujengwa na Mungu, jambo la msingi na kimetolewa na Mungu kutuwezesha ***"kuwasilishwa bila lawama na furaha kuu"*** mbele ya uwepo wake wa utukufu. (**Juda 24**).
Juda 20 ***"Bali ninyi, wapenzi, mjijenge juu ya imani yenu iliyo takatifu sana, na kuomba katika Roho Mtakatifu …"*** wakati tunapoomba katika lugha, roho yetu inakuwa inaomba kwa Mungu katika mawasiliano ambayo Yeye tu anafahamu (**1 Kor.14:2&14**). Hii ni njia moja ya msingi ambayo tunaweza ***'kuomba katika Roho***. Katika **a.18** Paulo anamshukuru Mungu kwamba ananena kwa lugha faraghani, maana hiyo ndiyo kusudi la kipawa hicho. Kukiwa na ujumbe katika lugha kwa ajili ya kanisa [ndimi kwa ajili ya kusanyiko], lazima kuwe na mtafsiri (**1 Kor.14:27-28**).

JINSI YA KUPOKEA UBATIZO KATIKA ROHO MTAKATIFU

1. *Tamani kujazwa* kikamilifu na Roho wa Mungu
Zab.42:1-2 ***"Kama vile ayala aoneavyo shauku maji ya mito, vivyo hivyo ndivyo nafsi yangu yakuonea kiu, Ee Mungu. Nafsi yangu inamkushaukia Mungu aishiye."***
Matt.5:6 ***"heri wenye njaa na kiu kwa ajili ya haki, maana watashibishwa."***
2. *Amini* kuwa utapokea Roho
Mk.11:24 ***"Yoyote muombayo mkisali aminini ya kwamba mnayapokea nayo yatakuwa yenu."***
3. *Njoo mahali pa maombi* kupiga magoti, kuketi, kusimama ama kilicho kizuri nawe. Ikiwa mtu amesimama, ni vyema mtu asimame nyuma yake ikiwa anaweza kuanguka kwa alili ya nguvu za Roho. Hata hivyo, mtu anapoanguka katika uweza wa Roho, haimaanishi amejazwa.

Tafuta kuona kama kuna ushahidi wa maandiko kuhusu kenena kwa lugha mpya ama kutabiri na kumtukuza Mungu.

4. *Abudu Bwana na kumshukuru*

Jihadhari na hali zo zote za usumbufu na ujaribu kusahau yale yanayotendeka karibu nawe. (**Zab.100:4**)

5. *Omba Mungu kwa ajili ya Roho na umshukuru kabla ya kujazwa*

Lu.11:13 ***"Basi ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vilivyo vyema, je, Baba wa mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu wale wamwombao."***

6. *Mshukuru na kumsifu kwa sauti*.

Sauti yako ndiyo inena hata wakati unanena kwa lugha, kumtazama Yesu ndio ufunguo maana yeye ndiye anayebatiza kwa kila kipawa, na Roho Mtakatifu. **Ebr.13:15**

7. *Tarajia kitu Fulani kutendeka*

Tarajia maneno mapya yaje kwenye kinywa chako, hisia kamili ya uwepo wake. Tarajia kumpokea Roho kwa kunena katika ndimi, unabii ama maono. Yawezekana kuwa na ajabu kwako lakini tenda katika imani. Ukimwangalia Yesu, ukimtumania Bwana.

Yoh.2:5 ***"Whatever He says to you, do it."'***

Matendo 5:32 ***"Na Roho Mtakatifu ambaye Mungu amewapa wote wamtiio."***

8. *Weka macho yako kwa Yesu*

Yeye ndiye anayebatiza katika Roho Mtakatifu.

Roho Mtakatifu hatakuwa kinyume na uamuzi wako; Atakujaza tu kulingana na kuamini kwako na kumwamini na kumtii. (**Matt.14:28-29**)

Sasa ni wakati wako wa kumwamini Mungu ili akujaze Roho Wake na kinywa chako na sifa; bila kujaribu kujua aina ya lugha ya mbinguni itakayo toka katika kinywa chako; kuingia katika ulimwengu wa Kiungu, kwa kuongea, kuamini, kuingia katika Roho wa Mungu ambao kila wakati ni maeneo mapya.

SURA YA TANO
KARAMA ZA ROHO

Kama sehemu ya Mwili Wake, kuna karama tofauti ambazo zinapatikana kwa ajili yetu: hasa karama za **1 Kor.12:8-10**.

1 Kor.12:4-6 ***"Basi, pana tofauti za karama; bali Roho ni Yeye Yule. Tena pana tofauti za huduma na Bwana ni Yeye Yule; tena pana tofauti ya kutenda kazi bali Mungu ni Yeye Yule azitendaye kazi zote katika wote."***

Tunapoomba na kuabudu pamoja Roho Mtakatifu anatuwezesha kutumia mojawapo ya hizo karama ama zaidi kwa ajili ya kujenga, kuhimiza na kutia nguvu wapendwa ambao wamekusanyika.

Karama za Roho: maana,

Kiyunani: *'pneumatikos'*, ***"kiroho"***, kile ambacho ni cha Roho ama kinachotokana na Roho;

tafsiriwa: - karama, dhihirisho, kuweka, uguzo, kinachotokana, kufunikwa, vitu, msaada, kazi, neema ama kibali cha Roho Mtakatifu.

'Charisma', ***karama ambayo inapeanwa kwa ukarimu,*** kwa nguvu zisizo za kawaida na baraka; kuwezeshwa na Roho au fadhili.

KARAMA ZA ROHO

1 Kor.12:1 ***"Basi ndugu zangu, kuhusu karama za Roho sitaki mkose kufahamu."***

1 Kor.12:4-6 ***"Basi pana tofauti za huduma na Bwana ni Yeye Yule. Kisha pana tofauti za kutenda kazi bali Mungu ni Yeye Yule azitendaye kazoo zote katika wote."***

MAELEZO YA KARAMA KATIKA 1 KOR. 12

NENO LA HEKIMA

a.8 ***"Maana mtu mmoja kwa Roho hupewa Neno la hekima"***

Kiyunani (Gr. *'spohia'* – maarifa yaliyo kamili ama ya juu sana; ujuzi katika kufanya matumizi ya kweli ya maarifa.

Mithali.3:13 ***"Heri mtu Yule aonaye hekima, na mtu Yule apataye ufahamu."***

Mithali.8:11 ***"Maana hekima ni bora kuliko maarifa wala vyote vinavyotamanika havilingani nayo."***

Yakobo 1:5 ***"Lakini mtu wa kwenu akipungukiwa na hekima na aombe dua kwa Mungu awapaye wote kwa ukarimu wala hakemei, naye atapewa."***

Yakobo 3:17 ***"Lakini hekima itokayo juu kwanza ni safi tena ni ya amani, ya upole tayari kusikiliza maneno ya watu, imejaa rehema na matunda mema, haina fitina, haina unafiki."***

Hii ni hekima itokayo kwa Mungu, sio hekima ya mwanadamu, kutembea katika Kristo, katika hekima Yake, tukijua kile ambacho Mungu atafanya katika hali Fulani kwa ajili yetu. Karama hii nafaa sana katika kushauri, lakini katika hali yo yote, tunaweza kumwomba Mungu kwa ajili ya Neno la hekima katika hali ama hitaji au mwelekeo wa mkutano.

Kwa mfano: Jawabu lake Yesu katika **Yohana.8:7** ni Neno la ajabu la hekima ambalo lilisawazisha hali iliyokuwa ngumu.

Matendo 4:19-20 jawabu la Petro na Yohana hapa pia ni mfano wa Neno la hekima katika hali iliyokuwa ngumu.

Mfano wa Neno la hekima ambalo linapeanwa na Roho na ambalo husuluhisha jambo lenye utata kwa ajili yetu: tulikuwa tukipanga kwenda Kenya kwenye safari ya huduma ya muda mfupi, mwaka wa 2000. Hata hivyo, tukapata mwaliko wa kwenda Myanmar ambako tulikuwa tumehudumu huko mara kadhaa. Safari ya Myanmar haikuwa ya gharama nyingi; tulijua hali ya huko na wapendwa wengi ambao ni wa kutegemewa katika kanisa. Afrika ni

ya kuvunja moyo, bila kujua safari mpya iliyo ghali na ilikuwa ikisemekana Kenya kuna hatari! Tukafanya maombi kwa Bwana kwa ajili ya Neno la Hekima ili kutangua kitendawili hiki. Bwana akweka uhai Neno katika **Matendo 16** ambapo Paulo alikuja Troa. Tulipoangalia kujua vile mstari wa **a.6b** unavyosema, ***"walikatazwa na Roho Mtakatifu kuhubiri Neno Asia."*** Tukashawishika kikamilifu kuwa Mungu wakati huu alitaka twende Kenya. Tukawa na ujasiri wa Kimungu kutoka saa ile.

NENO LA MAARIFA

a.8 ***"Maana mtu mmoja kwa Roho hupewa Neno la Maarifa"***

Kiyunani. *'gnosis'* – kile kinacho julikana ama kufahamika; kwa Neno la maarifa, Mungu anashiriki nasi sehemu ya maarifa Yake makamilifu; kujua jinsi Yesu angejulishwa katika hali kama hiyo.

Yesu alikuwa na Neno la Maarifa kuhusu mwanamke pale kisimani, **Yoh.4:16-19**.
Neno la maarifa linaweza kuja kwa njia ya wazo, hisia, maono, ama sauti inayokuzungumzia kuhusu hali Fulani. Ni Roho Mtakatifu anayenena nasi (**Yoh.16:13**).

Neno la maarifa mara nyingi hufichua hali Fulani za uponyaji. Bwana atafichua hitaji la uponyaji kwa mtu ambaye anahudumu na mtu huyo akiitikia kwa ujasiri wa matarajio, Bwana ataponya. Katika hali zingine za huduma hasa kufikia waliopotea, Bwana atafichua jambo kuhusu huyo mtu. Unaposhiriki lile ambalo Bwana amefichua, mtu huyo atashangaa na kustaajabu, 'ulijuaje kuhusu hilo jambo?' hali hii itamfungua huyo mtu kupokea Neno la Mungu zaidi.

KARAMA YA IMANI

a.9 ***"na mwingine imani katika Roho yeye yule"***

Kiyunani. *'pistis'* – Kuamini katika utendaji, ujasiri, tumaini, kuwa na hakikisho dhabiti la nguvu za Mungu, ukweli n.k.

Hii ni karama ya Roho kutoka kwa Roho Mtakatifu. Ni tumaini la Kimungu juu kupita imani, kutenda matendo ya Mungu, ***"imani ya Mungu".*** Hii ni karama ya rohoni kutoka kwa Roho Mtakatifu; sio karama ya imani iletayo wokovu (**Efe.2:8**). Tunahitaji karama ya roho ya imani wakati ambapo Mungu aepeana maono ama neno la kufanya jambo Fulani na hatuwezi kufanya; tunahitaji imani wastani; karama ya imani. **Mk.11:22** ***"Yesu akajibu akawaambia, Mwamini Mungu'."*** Ni kuwa na uhakika wa Mungu kwamba Roho Mwenyewe atapeana miujiza.
Matt.8:8-9 Mtu chini ya mamlaka: alikuwa nah ii karama?
Katika maombi kwa uponyaji na mafuta ya upako **Yakobo 5:15** yasema, ***"maombi ya imani yatamponya mgonjwa"***. Hii hakika sio imani ya kuamini na kuokoka kwa sababu hapa mwamini ndiy anayeitwa kuja katika uponyaji. Hili ni ombi ambalo linahitaji karama ya imani, kuwawezesha wazee wanaoomba kuamini kwa ajili ya uponyaji wa Kimungu kwa huyo mtu.

KARAMA YA MAPONYAJI

v.9 ***"Na mwingine karama za uponyaji katika Roho Yule mmoja"***

Kiyunani. *'iama'* – tiba, suluhisho Fulani kwa maradhi fulani.
Imeandikwa kama 'karama za maponyaji' katika wingi, kuonyesha kwamba Mungu anazo njia tofauti katika kuhudumu uponyaji. Hii karama yaweza kuwa yenye nguvu na iliyo juu katika kuwashawishi watu kumhusu Yesu na Injili Yake. Wagonjwa wanaponya kwa njia ya Mungu kupitia kwa karama hii.

Mk.16:18 inaonyesha kwamba kwa uponyaji kuna ukombozi wa wakati, ***"watapata kupona"***. Usikufe moyo ikiwa uponyaji hautafanyika mara moja. Ikiwa itatendeka mara moja ni muujiza. Wakati wa kuwaombea wagonjwa, omba kwa imani bila mashaka ukitarajia Roho

Mtakatifu kudhihirisha uwezo wake kwako ama Yule unayemwombea. Kwa mfano utaweza kuhisi moto mikononi mwako ama usiweze kuhisi, lakini mtu ambaye anaombewa atahisi joto. Hii ni njia amabayo inafahamika jinsi Roho anavyojidhihirisha, kuna njia zingine nyingi. Mara tu anapofahamu kwamba kumekuwa na dhihirisho la nguvu za Mungu, unaweza kushiriki kwa ujasiri katika imani kwamba huyo mtu amepona. Mara nyingi kutakuwa na unafuu kutokana na maumivu ama dhihiisho la uponyaji la kumtia moyo huyo mtu.

Yesu alipowatuma wale Thenashara kwenda kuhubiri katika **Matt.10:1**, Aliwapa uwezo wa kuponya kila aina ya magonjwa na maradhi; Aliwapa karama za maponyaji kwa Roho.

UTENDAJI MIUJIZA
a.10 *"Na mwingine matendo ya miujiza"* (matendo ya nguvu)
Kiyunani. *'energema'* – madhara, kudhihirisha, kusababisha kutendeka, matukio ya nguvu ya Mungu;
Kiyunani. *'dunamis'* – Matendo makuu, nguvu za miujiza, nguvu ambazo si zakawaida.

Utendaji wa miujiza unapita sheria zote za kiasili, ama mkondo wa mambo, ambao unaleta tukio kando na njia za kawaida.
Kuna mifano mingi ya miujiza ya Yesu. Tazama **Yoh.2:1-11** mfano mmoja.
Stefano alikuwa nah ii karama, **Matendo 6:8** ***"na Stefano akijawa na imani na uwezo alikuwa akifanya maajabu na ishara kubwa katika watu."***
1 Kor.12:28 inatwambia kuwa Mungu ameweka karama kanisani. Hizi pamoja na zingine mtu anaweza kupewa ili afanyike mtenda miujiza.

KARAMA YA UNABII
v.10 *"Na mwingine unabii"*
Kiyunani. *'propheteia'* – kunena kwa pumzi, kwa uweza wa Mungu ama ufunuo; yaweza kuhuzisha kutabiri, lakini sio kawaida; kunena maneno ya Mungu katika pumzi Yake.
Unabii ni katika lugha inayoeleweka na ni sawa na kutafsiri ndimi. Inajitokeza kwa njia ya hisia, mawazo, maono, sauti ya Roho, pamoja na kujua ama kuhisi kwamba hili ni la Mungu na sio mimi.

Hii karama inamsaidia mtu kunena kwa niaba ya Mungu. Mara nyingi mtu ambaye hutumia karama hii anakuwa amepokea sehemu tu ya yale ambayo Roho anakusudia kutenda. Mtu anahitaji kutamka kile ambacho wamepokea na karama itatiririka. Karama ya unabii ni ya kujenga, kuhimiza na kufariji. **1 Kor.14:3** ***"Bali yeye ahutubuye, asema na watu maneno ya kuwajenga na kuwafariji na kuwatia moyo."***

KUPAMBANUA ROHO
a.10 *"Na mwingine kupambanua roho"*
Kiyunani. *'diakrisis'* – kutofautisha, tendo la kuchunguza, kufahamu, kuchunguza, kutambua, kuelewa.
Hii karama ya kupambanua ni yenye macho ya kiroho, kuona yaliyomo katika ulimwengu wa Roho, kuona kile ambacho kinatendeka; huku ni kupambanua yale yanayoendelea katika Roho kama Yesu ageweza kufanya; ni kutofautisha kati ya mtu ambaye anawezeshwa na Mungu na Yule ambaye anajifanya kutumiwa.

> Tazama mfano katika **Matendo16:16-18** Paulo alitambua roho wa uanguzi ndani ya Yule msichana. Alionekana kuwa alikuwa akisema ukweli lakini kwa roho isyokuwa ya kweli.

Kuna himaya tatu [asili] ya Roho
1. ***Mungu Roho Mtakatifu na viumbe vya mbinguni***: Makerubi, Maserafi, viumbe vilivyo hai, malaika na watakatifu waliotukuzwa.
2. ***Shetanimalaika walioanguka na mapepo wachafu.***

3. ***Roho za wanadamu*** – kila mwanadamu anayo roho.

Kupambanua roho ni kujua roho gani inayofanya kazi. Je! Huyo mtu anatembea katika Roho Mtakatifu; je! Huyo mtu amepagawa; je! Huyo mtu anaiga akiwa katiak mwili? Hii karama inawezesha huduma ya ukombozi kutoka kwa roho mchafu kwa njia ya nguvu.

KARAMA YA NDIMI

a.10 *"Mwingine aina ya lugha"*

Kiyunani. *'genos'* – hesabu ya hali nyingi.

Kiyunani. *'glossa'* – ndimi, lugha yo yote; lugha ambayo mtu hakufahamu awali, anayonena kwa kuongozwa na Roho.

Kunena katika ndimi ni ishara ya kwanza ya kubatizwa katika Roho Mtakatifu na kunaushahidi wa Maandiko kuhusu jambo hili kuwa tofauti na yanayofundishwa katika **1 Kor.12**. karama za ndimi zinazopokewa wakati wa ubatizo kwa mtu katika Roho Mtakatifu ni ya maombi kwa Mungu faraghani kwa ajili ya kujijenga binafsi na hakuhitaji kutafsiriwa wakati zinapotumiwa katika maombi ya binafsi(**1 Kor.14:2,4**).

Karama ya ndimi tofauti ni ya Roho Mtakatifu kuleta ujumbe katika kusanyiko la watu wa Mungu. Ujumbe katika lugha isiyojulikana inahitaji kutafsiriwa. Roho Mtakatifu anapompa mtu ujumbe kwa ajili ya mkutano kwa lugha isyofahamika, anafanya hivyo ili kila mtu amakinike, kwa sababu tafsiri wakati wote huendeshana pamoja na karama ya unabii.

Matumizi mengine ya karama ya ndimi ambayo inajidhihirisha hata leo, ni kumwezesha mtu kushuhudia injili ya Bwana wetu Yesu Kristo katika lugha ambayo sio ya kawaida. Kwa mtu anayeijua hiyo lugha.

KARAMA YA KUTAFSIRI LUGHA/NDIMI

v.10 *"Na mwingine tafsiri ya lugha"*

Kiyunani. *'hermeneia'* – tafsiri ama maelezo.

Tafsiri ya lugha huleta maana ama ufahamu way ale ambayo yananenwa katika lugha, wakatika mwingi sio neno kwa lingine kwa sababu hii sio lugha wya wanadamu. Inaweza kuja kama wazo, ama maono na inaweza kuja kwa njia ya mtu mmoja ama zaidi na wakati inapotumiwa na kushiriki inaweza kukubalika. Katika maombi ya kikundi, ujumbe unaoletwa katika lugha unawafanya watu kumakinika; kisha kusanyiko linangojea Mungu kuwachilia tafsiri yake; hili huwezesha kuleta mwelekeo wa mkutano.

Kunena katika ndimi na kutafsiri ndimi ni kara yenye nguvu zinapojidhihirisha katika mkutano wa kanisa. Kwa bahati mbaya, kwa sababu ya kuchanganyikiwa katika ufahamu wa wengi kuhusu 'kunena katika ndimi', wakristo wengi hawajawahi kuwa kwenye mikutano ambapo karama hizi mbili zinahudumu.

KUHUDUMU KARAMA

Watu wa Mungu wanatakikana kuhimizwa kwamba kupokea na kuhudumu katika karama za Roho Mtakatifu ni rahisi. Mazoezi ya mema ni kukusanya watu katika kikundi kidogo baada ya kuwapa mwelekeo juu ya karama na kuwauliza waombe kwa zamu. Kikundi chote kingojee Roho kwa ajili ya karama. Hivi majuzi katika kikundi kama hicho, wasichana wa umri wa miaka 9 na 10 walipokea karama na wakaweza kuhudumu; mmoja alikuwa akitabiri na mwingine akapokea maono Fulani. Sio sana katika kutumia kwetu karama, lakini ka kwa ajili ya kujitolea kwa Roho Mtakatifu anaweza kututumia.

Karama Tisa za 1 Wakorintho 12 zinaweza kuwekwa katika makundi matatu:

1) Karama za mawasiliano: Unabii, Ndimi, Tafsiri ya ndimi

Kuyanena mambo kwa njia ya Kimungu, huu ni ***unenaji wa Roho Mtakatifu***
Kuwezeshwa kujieleza na kuwasilisha mawasiliano ya miujiza kwa Neno; Pumzi ya Mungu; maneno.

2) KARAMA ZA UFUNUO: Hekima, Maarifa, Kupambanua
Kuyajua mambo kwa njia ya Kiungu; ***akili za Roho Mtakatifu***
Kuwezeshwa kuelewa na kuona
Miujiza kwa mawazo; habari; ukweli

3) KARAMA ZA KUONYESHA: Miujiza, Maponyaji, Imani
Kuyafanya mambo kwa njia ya Kiungu ***okombozi kwa Roho Mtakatifu***
Kuwezeshwa kwa nguvu na uwezo
Miujiza katika matendo; Tendo; matendo

KATIKA UPENDO
Shemu ya upendo katika kutumia karama (**1 Kor.13**) inakuja katika mafunzo ya Paulo katika kutumia karama za Roho, ***"bila upendo, mimi si kitu"*** (**a.2**). Upendo unastahili kuwa kitu cha kutuchochea na lengo la kuhudumu katika karama. Pasipo nguvu za Roho Mtakatifu, upendo huu, yaani Mungu ni upendo ndani yetu na kwa njia yetu, hautafanya kazi. Tuahita hizi karama ili tukaweze kuhudumu upendo Wake kikamilifu. Bila upendo, tunaishi chini ya hukumu(**Matt.7:19-23**).

Kuhudumu karama ni kumuhudumia mtu mwingine ama kikundi; kuna njia nyingi ambazo karama zinaweza kuhudumu. Anayepeana anapokea sifa na utukufu wala sio mtumishi.

NGUVU ZA MUNGU
Kwa njia ya hizi karama, Roho Mtakatifu anatufanya tuwewashirika wa nguvu za Mungu; kama kristo anavyotufanya washirika wa uungu wake kwa njia ya Neno Lake (**2Pet.1:4**). Mungu Baba anaafikia lengo Lake kunapokuwa na mtiririko wa nguvu zake; tunamtumikia Bwana Yesu Kristo tunaposhirikiana na kuhudumu katika karama ambazo tumepewa na Roho Mtakatifu Mungu katika utatu mkamilifu ukishirikishwa.

SURA YA SITA
KUKAZA MWENDO KUFIKIA UTIMILIFU

Kazi ya karama za Roho katika kuleta kanisa katika utimilifu
Ebr.6:1 *"Kwa sababu hiyo, tukiacha kuyanena mafundisho yakwanza ya Kristo, tukaze mwendo na tuufikilie utimilifu....."* huu utimilifu ni ukomavu, ukamilifu, ukamilifu ambao kanisa linatakikana kufikia katika Kristo Yesu.

Paulo anaelezea kuwa Yesu kama Mume na kanisa kama Bibi arusi ambaye ana andaa ili awe ***"tukufu bila mawaa"*** (**Efe.5:22-27**).
Efe.5:25 ***"Kristo alilipenda kanisa hata akajitoa kwa ajili yake;***
a.26 ***kwa kusudi alitakase na kulisafisha kwa maji ya neno,***
a.27 ***Apate kujiletea kanisa tukufu lisilo na ila wala kunyanzi wala lo lote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa."***

Neno*"kanisa"* (Kiyunani: *'ecclasia'*) lamaanisha "walioitwa na Mungu" na ni Kristo ***"ndiye awezaye kuwalinda ninyi msijikwae na kuwasimamisha mbele ya utukufu wake bila mawaa na furaha kuu."*** (**Juda 24**)

KANISA LINAWEZAJE KUUFIKIA UTIMILIFU?
Waraka kwa Waefeso unafundisha: juu ya utimilifu;
i. wa Kristo na kanisa;
ii. Kristo katika ulimwengu wa Roho akitimiza makusudi ya Mungu na kudhihirisha kusudi Lake hapa duniani kwa njia ya kanisa.
iii. wa huduma za karama za Yesu katika Wefeso 4 kufanya Mwili wa Kristo wote ukafikie ukamilifu.

Efe.4:1 inafundisha jinsi ya ***"kuenenda iasavyo mwito tulioitwa."***
Efe.4:8 kuwezesha kanisa kuhudumu katika ukamilifu; Yesu aliyefufuka ***"aliwapa watu vipawa."***
Hivi vipawa vilivyonakiliwa katika **a.11**, vinajulikana kama vipawa Vyake Kristo aliyefufuka na Kupaa. Ni Kristo aliyefufuka na kuketishwa ***"mkono wa kuume wa Mungu katika ulimwengu wa Roho"*** (**Efe.1:20**) ndiye anayepeana vipawa hivi.
Efe.4:11 ***"Naye alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii, na wengine kuwa wainjilisti , na wengine kuwa wachungaji na waalimu."***

Kwa Nini Yesu Alitoa Vipawa Hivi?
Efe.4:*12* ***"kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu***
Hata kazi ya huduma itendeke,
Hata mwili wa Kristo ujengwe."

Lengo ni nini?
Efe.4:13 ***"hata sisi sote tuufikie umoja wa imani***
Na kumfahamu sana Mwana wa Mungu,
Hata kuwa mtu mkamilifu,
Hata kufikia cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo." (**fananisha na. Efe.1:22-23**)
Efe.4:14 ***"Ili tusiwe watoto wachanga tena"*** lakini tukuwe tukiwa na mizizi katika imani na kusimamishwa kwenye Neno.

Haya yatatimizwa kwa njia gani?
Efe.4:15 ***"Lakini tushike kweli katika upendo,***
Na kukua hata tumfikie yeye katika yote katika yote, yye aliye kichwa, Kristo"-

Efe.4:16 ***<u>"Katika yeye mwili ukiunganishwa na kushikamanishwa kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadri ya utendaji wa kila sehemu moja moja, huukuza mwili upate kujijenga wenyewe katika upendo</u>."***

Ni jinsi kanisa linavyopkea na kuruhusu hivi vipawa vitano kutenda kazi ya kwamba likakuwe hata kufikia utimilifu.

Mtume Anafanya Nini?

Mtume ni mjumbe maalum, aliyetumwa na Kristo amwakilishe (**Matt.10:40**) kwa Neno na ishara zikifuata. Mitume wameitwa na Kristo na kupewa wajibu maalum wa kujenga kanisa, nyumba ya Mungu. Mtume anaujasiri wa kumkiri Yesu, na huendelea katika kutimiza Tume Kuu, kupanda makanisa na kuwakuza watenda kazi kuhudumu katika makanisa hayo. Paulo anasema mtume ni mjenzi mwenye hekima (**1 Kor.3:10**).

Mtume amepewa ufahamu wa siri ambazo Mungu anataka watakatifu wajue. Mtume hupanua kazi ya kanisa kwa kuingia katika maeneo mapya kwa injili. Kanisa ambalo huduma hii inafanya kazi ni kanisa linaloonekana; kanisa ambalo linahusika na kuwafanya wanafunzi na kuwakusa watenda kazi kwa ajili ya mavuno; kanisa ambalo linafikia mataifa.

Kazi Ya Nabii Ni Gani?

Nabii ambaye amewekwa katika kanisa na Yesu ni msemaji wa Mungu katika njia Fulani. Huyu mtu husikia na kisha huleta ujumbe ambao ni wa Mungu kwa ajili ya kanisa. Wakati karama hii inafanya kazi, kanisa hujulishwa mapenzi ya Mungu na jinsi anavyotaka hayo mapenzi yafanyike. Nabii wakati mwingine anakuwa na kipawa cha kujua mambo ya siku za usoni. Sauti ya kinabii katika mkutano wa maombi una nguvu ya kuelekeza mkutano. Hii karama huambatana na kipawa cha unabii.

Mungu alimwamba Amosi: **Amosi 3:7** ***"Hakika Bwana hatafanya jambo lo lote bila kuwafunulia watumishi wake, manabii siri yake."*** Yesu alisema Roho ***"atawajulisha mambo yatakayokuja."*** (**Yoh. 16:13**)

Kipawa cha unabii hususan ni cha kuelekeza kanisa. **1 Kor.14:1** ***" tafuteni sana karama za rohoni lakini zaidi kwamba mkaweze kuhutubu."*** Musa pia alitambua hitaji la kuwa na mwongozo wa kimungu.

Hesabu.11:29 ***"Heri watu wote wa Bwana wangekuwa manabii, na kama Bwana angewatia Roho Yake."***

Kazi Ya Muinjilisti Ni Gani?

Hiki kipawa hupewa watu wengine ambapo kupitia kwa hicho kipawa waamini huja kupata wokovu kwa njia ya kuhubiri na kushuhudia. Muinjilisti anaondoka kanisani kufikia jumuia. Waumini wapya kisha huletwa kanisani ili watunzwe na mchungaji na mwalimu. Huduma ya Filipo katika Samaria, na Yule Mkushi, na katika miji mingi katika **Matendo 8** ni mifano yenye nguvu ya uinjilisti.

Kazi Ya Mchungaji Ni Gani?

Kimsingi mchungaji hulisha na hutunza watu wa Mungu katika Mwili wa Kristo. Anatimiza tume Yesu alimpa Petro alipomwambia ***"Tunza kondoo wangu."*** (**Yohana 21:16**) yeye hatunzi tu watu bali pia Neno la Mungu. Mtume Paulo akiwahutubia wazee [wachungaji] wa kanisa lililoko Efeso katika **Matendo 20** na katika **a.28** anawambia wachunge kundi la Mungu ambalo wamewekwa kuwa waangalizi. Mtume Petro pia aliwapa wazee ushauri uo huo katika **1 Pet.5:1-4**.

Kazi Ya Mwalimu Ni Gani?

Mwalimu katika kanisa huonyesha ukweli. Karama maalum ya kufundisha imetolewa ili iweze kuleta ufunuo wa Neno. Watu ambao wanakaa chini ya mafundisho yenye upako hupata ***"macho ya ufahamu wao yanatiwa nuru."*** (**Efe.1:14**) Neno linaloletwa na mwalimu

mwenye upako huponya, huokoa, hukomboa na huweka huru waliosetwa. Mara nyingi wachungaji huwa na kipawa cha kufundisha na hakika kila mchungaji [mzee katika Agano Jipya] anahitaji kujua kufundisha Neno la Mungu.

Uzima Katika Kanisa La Kwanza.
Tunawaona viongozi wa kanisa la kwanza wakitembea katika karama hizi za Kristo aliyepaa kwa ajili ya kujenga kanisa.
1 Tim.4:14 Wazee walimwekea Timotheo mikono, wakanena maneno ya unabii juu yake na wakamwekea kipawa.
2 Tim.1:6 Paulo anamuusia Timotheo ***"kuchochea karama iliyomo ndani yako kwa kuwekewa mikono yangu."***
Kupita kuwekewa mikono, watu ***"waliojaa RohoMtakatifu na hekima"*** walitengwa kwa ajili ya huduma. (***Matendo 6:6***)
Matendo 13:3-4 baada ya kuwekewa mikono, ***"walitumwa nje na Roho Mtakatifu."***
Kanisa la kwanza lilipoendelea ***"kudumu katia fundisho la mitume na katika ushirika"*** (**Matendo2:42**), ***" Bwana alisidisha kanisa kla siku wale waliokuwa wakiokoka kila siku."*** (**Matendo 3:47**)

Huduma ya "kipawa" huzaa huduma kwa "kila sehemu".
Paulo anatwambia tutamani nini?
1 Kor.14:1 ***"Fuateni upendo na kutafuta na kutaka sana karama za rohoni lakini zaidi mpate kuhutubu."***
Mbona tunahimizwa kuhutubu?
a.3 ***"yeye ahutubuye anasema na watu maneno ya ya kuwajenga na kuwafariji na kuwatia moyo."***
Kwanini inatupasa kutamani vipawa vya rohoni?
a.12 ***"ili kulijenga kanisa."***
Ni vipawa gani tunastahili kutarajia wakati tunapokuja pamoja?
a.26 ndimi na tafsiriyake, mafunzo na ufunuo, saburi.
Kwa nini tuviweke katika utendaji?
a.26 kwa kujenga na kuhimiza Mwili wa Kristo.
Kol.3:16 ***"Neno la Kristo na likae ndani yenu kwa wingi katika hekima yote, mkifundishana na kuonyana kwa saburi na tenzi za rohoni huku mkimwimbia Bwana mioyoni mwenu."***

Kama sehemu ya Mwili wa Kristo tukihudumiana mmoja kwa mwingine, Bwana anatukuzwa.

Huduma Ya Agano Jipya.
Kanisa [watu wa Mungu walioitwa] wanategemea Roho kwa ajili ya kupokea vipawa vya Mungu.
2 Kor. 3:5 yatwambia ***"utoshelezi wetu watoka kwa Mungu."***
a.6 Mungu ametufanya kuwa ***"wahudumu wa Agano Jipya"***
a,6 amefanya haya sio kwa ***"waraka bali kwa Roho***
a.6 ***"Roho anahuisha."***
a.8 huduma ambayo Roho anapeana ***"ni huduma ya utukufu."***
Tunapoendelea katika huduma ya nguvu za Roho Mtakatifu ***"tuanabadilishwa na kufanana na mfano uo huo toka utukufu hadi utukufu."*** **2 Kor.3:18**
It is as we believe that we speak. **2 Kor.4:13** ***"I believed, therefore I spoke."***
Therefore ***"knowing the fear of the Lord, we persuade men."*** **2Kor.5:11**
Paulo anaiita huduma ambayo tumepewa *huduma ya kuupatanisha ulimwengu,* **2Kor.5:18**
Tumeitwa tuwe ***"wajumbe wa Kristo."*** **2Kor.5:20**

Tumia Vipawa Vya Kiroho
Ili uwe mhudumu wa Agano Jipya ambalo kwalo tumeitwa, inatubidi tutumie vipawa vya Kiroho ambavyo ametupatia.

1Pet.4:10 ***"Kila mmoja kwa kadri alivyopokea karama, aitumie kwa kuhudumiana kama mawakili wema wa neema mbali mbali za Mungu.***

1Pet.4:11 ***"Mtu akisema na aseme kama mausia ya Mungu, mtu akihudumu na ahudumu kwa nguvu anavyojaaliwa na Mungu ili Mungu atukuzwe katika mambo yote kwa Yesu Kristo. Utukufu na oweza una Yeye hata milele na milele. Amina".***

Rum.12:4-5 ***"kwa kuwa kama vile katika mwili mmoja kuna viungo wala viungo vyote havitendi kazi moja, vivyo hivyo nasi pia tulio wengi, tu mwili katika Kristo na viungo kila mmoja kwa mwenzake.***
a.6 ***"Basi kwa kuwa tuna karama zilizo mbali mbali kwa kadri ya neema tuliyopewa … wacha tutumie … in kwa kadri ya imani."***

Karama Za Mungu Ni Za Kimsingi Kwa Kanisa
Yatupasa kuzitamani, kuzitafuta, kuzipokea na kuzitumia ***"ili tujenge mwili wa Kristo"*** (**Efe.4:12**) ili mwili wake ***"uwe umekamilika kwa yote katika yote."*** (**Efe.1:23**)

Katika siku hizi, Mungu anarejesha vipawa vitano vya huduma kwa kanisa,
Na hata sasa tunashuhudia urejesho wa huduma ya kiutume.

SURA YA SABA
KARAMA SABA ZA BABA KATIKA RUM. 12

Kuna makundi matatu katika Agano Jipya na pia kuna kundi la pamoja katika **1Kor.12:28**. Orodha tatu hizo zinaweza kuonekana zikiwakilisha Utatu Mtakatifu wa Mungu.

1. ***Karama tisa za Roho Mtakatifu*** **1Kor.12:8-10**. Hisi karama zinapeanwa na **Roho Mtakatifu** kwa waaminio **a.4** na hudhihirishwa na Roho Mtakatifu kwa manufaa ya wote.
2. ***Karama tano za huduma*** **Efe.4:11** zinapeanwa na **Yesu Kristo** kwa ajili ya kulikamilisha kanisa.
3. ***Karama saba za uumbaji [uchochezi] za*** **Rum.12:6-8** zinapeanwa na **Baba** wakati wa uumbaji wa viumbe vyake vyote. Paulo anapozungumzia karama hizi kutofautiana kulingana na neema, na hudhihirishwa kwa neema ya Mungu ***"huwamwagia wenye haki na wasio haki".*** Kwa maneno mengine hizi karama mtu huzipokea wakati wa kuzaliwa na katika kila jumuia, watu huenda katika karama hizi, wakihudumiana katika maisha yao. Mara mtu anapookoka na kujiunga katika mwili wa Kristo, karama za uumbaji hutekeleza kazi muhimu katika kuusababisha mwili kufanya kazi ipasavyo.

I Kor.12:4-6 inadhihirisha sehemu hizo tatu kama ifuatavyo:
1. **a.4** ***"Basi pana tofauti ya karama lakini Roho Mmoja"***; Hii inaashiria karama tisa za Roho Mtakatifu katika **1Kor.12:8-10**, ambazo zinapeanwa na Roho Mtakatifu kwa kila sehemu ya Mwili **a.11**.
2. **a.5** ***" Tena pana tofauti ya huduma, na Bwana ni Yeye yule"***; hii inaashiria karama tano ambazo zimepeanwa kwa kanisa na Yesu katika **Efe.4:11**.
3. **a.6** ***"Kisha pana tofauti za utenda kazi, bali Mungu ni yeye Yule azitendaye kazi zote katika wote"***; hizi ni karama ambazo ziko katika **Rum.12:6-8** na zimepeanwa na Baba Mungu.

KARAMA ZA BABA

Zinaitwa ***karama za uumbaji*** maana zinapeanwa wakati wa uumbaji. Hizi karama zinafanya kazi tofauti na zinadhihirisha karama za Rohoni katika **1Kor.12** na hizi orodha mbili ni tofauti katika utenda kazi ukilinganisha na karama za huduma za **Efe.4:11**. Kwa mfano, unabii umeorodheshwa katika **Rum.12** na **1Kor.12** na huduma ya nabii imeorodheshwa katika **Efe.4**. ingawa mtu anaweza kupokea hizi karama zote tatu bali ziko tofauti sana.karama ya kufundisha katika **Rum.12** na huduma ya Mwalimu iko katika **Efe.4**. hizi karama za kufundisha ni tofauti sana katika utenda kazi. Kusudi ya hili fundisho ni kuelewa karama za Baba.

Rum.12:4 ***"Kwa kuwa kama vile katika Mwili mmoja kuna viungo vingi, wala viungo vyote havitendi kazi moja."*** Kila kiungo kina kazi tofauti jinsi inavyosema **1Kor.12:6** ***"Kisha tofauti za kutenda"***. Hizi karama ni sehemu za kutenda kazi na mwanadamu katika jumuia.

UNABII

Inamaanisha nini kutabiri ukitumia kipawa hiki? Katika funzo lililomalizika, tuliona karama ya unabii kwa Roho Mtakatifu, na kwa kifupi tukaangalia kuhusu huduma ya nabii. Karama hii ya uumbaji ni tofauti sana kwa hizo mbili; ni kipawa ambacho ni cha 'asili' cha kuangala ndani; mtu ambaye anapambanua mambo sawasawa katika hali Fulani, mtu ama shida. Kwa maneno mengine, huyu ni mtu ambaye anaweza kunena hekima na kutoa ushauri unaofaa, sio kwa karama ya Roho, ama kutokana na huduma kama nabii lakini kupitia kwa kipawa cha asili. Watu wengine ni manabii kiasili; wanachunguza kwa ndani kwa sababu Mungu amewapa karama hiyo.

Rum.12:6 ***"Tabiri kwa kadri ya imani"***; ikiwa unaamini umepewa kipawa hichi, basi shiriki na watu wanaostahili.

HUDUMA ama UTUMISHI

Watu wengine hupata ni rahisi kutumika, kuhudumia mahitaji yaw engine. Watu walio na kipawa hiki wanaona kile ambacho kinatakikana kufanyika na wao hukifanya. Hiki kipawa hudhihirika sana katika huduma ya usaidizi kulingana na Maandiko, na yaweza kufanana na huduma ya ***"masaidiano"*** katika **1 Kor.12:28**. Wengi wetu inafaa kuulizwa kutumika lakini wengine ni jambo la kawaida.

Rum.12:7 ***"tuwemo katika huduma yetu"***; kunahuduma ambayo inaweza kutusaidia kuhudumia wengine.

KUFUNDISHA

Mtu ambaye kiasili anapenda kuwafafanulia watu mambo, kutamani kuwapa watu maarifa. Watu wengi ambao huchagua kufundisha kama taaluma, wanakarama hii ya hisia katika maisha yao kutoka kwa Mungu, na watakuwa waalimu wazuri.

Rum.12:7 ***"Mwenye kufundisha katika kufundisha kwake*** pia, ikiwa una kipawa [haja ama hisia] ya kufundisha, itambue na uitumie kwa kufundisha. Inaweza kumaanisha kuwafundisha watoto ama wakristo wachanga kanisani.

KUONYA

Kuonya nikutia moyo, kuwajenga watu wengine. Ni nani anayependa kutiwa moyo? Je, unajua mtu yeyote ambaye anapenda kukitumia kipawa cha kuwatia moyo wengine? Sote tunaweza kupokea kipawa hiki kwa neema. Jina Barnabas linamaanisha ***'mwana wa kuta moyo'*** (**Matendo 4:36**) na tunamuona Barnaba akitumia kipawa hiki kwa Sauli [Paulo] katika huduma.

Rum.12:8 ***"Mwenye kuonya katika kuonya kwake"***; tumia kipawa ambacho umepewa na Mungu kwa kuwajenga wengine – sote tunahitaji kujengwa katika njia moja ama nyingine.

KUKIRIMU

Watu wengine ni wakarimu tu kwa kuzaliwa; watu wengine ukiwatembelea lazima wakupatie kipawa. Viungo vya Mwili vinaweza kutegemewa kwa ajili ya kukirimu sehemu zingine za mwili. Sio katika kifedha tu, kwa sababu wale walio na kipawa hiki hata bila pesa watakupatia kipawa cha aina yo yote.

Rum.12:8 ***"Mwenye kukirimu, kwa moyo mweupe"***; Yesu ametuahidi ***"wapeni watu vitu nanyi mtapewa; kipimo kizuri, kilichosindiliwa, kilichosukwasukwa na kumwagika watu watawapeni vifuani mwenu. Kwa maana kile kipimo ipaimiacho, ndicho utakacho pimiwa wewe."***

UONGOZI

Watu wengine ni viongozi wa asili. Katika kikundi cho chote ama kazini, ni lazima kuwe na kiongozi. Sukuru Mungu kwa hiki kipawa ili tusiende katika mviringo tukitanmani mtu atupatie mwongozo.

Rum.12:8 ***"Mwenye kuongoza, aongoze kwa bidii"***; kiongozi anatakikana kutekeleza kazi yake kwa bidii.

KUREHEMU

Kipawa cha huruma kinadhihirishwa kwa Yule aliye nahitaji; kuambatana na mtu katika hali yake ili umsaidie has asana wakati hawastahili kuhurumiwa.

Rum.12:8 ***"Mwenye kurehemu kwa furaha"***; sio kwa kulazimishwa bali kwa furaha.

TAMATI

Kila mtu angalau anamoja ya hizi karama ambayo huchochea tabia na na kila mara kuadhiri maeneo ya kazi ama taaluma ambayo wanajitolea kuifanya. Kwa mfano, watu wenye karama ya kurehemu utawakuta wakifanya kazi katika kutunza watu kama wauguzi. Kila jamii na jumuia ya watu na kila ushirika wa watu wa Munguyapasa wawe na hizi karama katika utenda kazi. Katika Mwili wa Kristo yatupasa kusaidia watakatifu kutambua maeneo yao ya huduma kulingana na **Rum.12:6-8** na kuwatia moyo kutumia vipawa vyao. Hii itakuwa ya manufaa katika kukusa na kuchapa kazi kikamilifu.

MATUMIZI

Katika vikundi vidigo vya watu wanaojuana, chukuwa muda kutambua hivi vipawa katika kila mmoja wenu. Ikiwa tutasimama na kufikiria kuhusu kila mmoja wetu, hivi karibuni tutaweza kutambua kwamba kila mmoja katika mwili anaenda ama kutembea katika moja ama zaidi ya hizi karama. Wakati mwingine mtu anakuwa anajua kipawa cha asili alicho nacho; wakati mwingine mtu anahitaji msaada kutoka kwa watu wengine ambao wanaweza kutambua kipawa cha hisia katika ndugu ama dada yao.